**Korti** Kuu yatengua hukumu aliyefungwa miaka 30 gerezani

UKURASA 3



**Aagiza** watumishi wasimamishwe kwa tuhuma ubadhirifu

UKURASA 3





# Nipashe

Ijumaa Julai 9, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580636

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US





UKURASA 11

# Samia awakatalia viongozi wa dini

UK. 2

## YALIYOMO


UKURASA WA 4

**VIKWAZO VYA BIASHARA NA KENYA KWISHA AGOSTI**

KENYA imesema vikwazo 30 vya biashara kati ya nchi yake na Tanzania vitapata ufumbuzi ifikapo mwezi ujao.

UKURASA WA 5

**MUHIMBILI YAHUDUMIA WENGI SABASABA**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH), imesema kati ya wananchi 2,000 waliotembelea banda la hospitali hiyo kwenye Maonyesho ya Sabasaba, 921 walifanyiwa uchunguzi na tiba.

UKURASA WA 5

**RC AWAOMBA VIONGOZI WA DINI VITA UBAKAJI**

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, amewaomba viongozi wa dini wawapo kwenye nyumba za ibada kukemea ....




Rais Samia Suluhu Hassan akisindikizwa na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT), Askofu Dk. Alinikisa Cheyo, baada ya kufungua Mkutano Mkuu wa Jumuiya hiyo, mkoani Morogoro jana.. **PICHA: IKULU**.

## NDC yabanwa kuilipa NSSF mabilioni

UKURASA 4

## Ndalichako ataka vyuo, shule kuzingatia mwongozo corona

UKURASA 2

**MICHEZO** **AZAM YAIMWAGIA YANGA MABILIONI** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

## Sababu JK, Mwinyi kuzuru SGR yatajwa

**Na Waandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mohamed Mchengerwa, amesema ziara ya siku mbili ya marais na mawaziri wakuu katika Mradi wa Bwawa la Julius Nyerere na wa ujenzi wa reli ya kisasa (SGR), iliandaliwa na Rais Samia Suluhu Hassan.

Amesema lengo la Rais Samia ni kutoa fursa kwa viongozi hao wastaafu wa kitaifa kuona maendeleo ya mchango walioutoa wakati wa uongozi wao na kuwapa fursa ya kushuhudia hatua ambayo serikali imefikia katika ujenzi wa miradi hiyo mikubwa ya kimkakati.

Mchengerwa alitoa kauli hiyo juzi mkoani Dar es Salaam baada ya viongozi hao wastaafu wa kitaifa kuhitimisha ziara yao ya kujionea maendeleo ya ujenzi wa miradi hiyo.

Waziri huyo alimpongeza Rais Samia kwa kuwaandalia ziara hiyo mahususi marais na mawaziri wakuu wastaafu ambao wakati wa uongozi wao walitoa mchango mkubwa katika kujenga misingi imara ya utekelezaji wa miradi hiyo ya kimkakati na yenye tija katika uchumi wa taifa.

Mchengerwa alisema marais na mawaziri wakuu wastaafu wamefurahi kuona mawazo na mapendekezo waliyoyatoa kuhusu utekelezaji wa miradi hiyo yamefanyiwa kazi kikamilifu na Serikali ya Awamu ya Tano na kuendelezwa na Serikali ya Awamu ya Sita.

"Mipango yote ya kuwa na miradi ya kimkakati ilianza wakati wa uongozi wa Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere na kuendelezwa na marais wote wastaafu na hivi sasa inaendelea kutekelezwa na Rais Samia Suluhu Hassan," alisema.

Akijibu swali la mwandishi wa habari kuhusu mchango wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora katika usimamizi wa utekelezaji wa miradi ya kimkakati, Mchengerwa alisema ofisi yake inahusika katika usimamizi wa miradi hiyo kwa kuwa wanaosimamia miradi hiyo ni watumishi wa umma ambao wameajiriwa na serikali ili kuwatumikia Watanzania.

Ziara hiyo ya viongozi wastaafu wa kitaifa iliwahusisha marais wastaafu Ali Hassan Mwinyi na Jakaya Kikwete, na mawaziri wakuu wastaafu; Cleopa Msuya, John Malecela na Mizengo Pinda.

**•Imeandaliwa Rausath Sued na Sabrina Omary, SJMC**



Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Adamu Malima (katikati), akizungumza na wadau wa zao la mkonge mkoani humo jana, ambapo alitoa maagizo ya kuangaliwa upya mkataba uliopo kati ya kampuni tanzu ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) ya Sisalana inayojihusisha na uchakataji wa zao hilo na wakulima wa vyama vya ushirika (AMCOS) wilayani Korogwe, baada ya vyama hivyo, kuilalamikia kampuni hiyo. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**

# Samia awakatalia viongozi wa dini

**Na Waandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema serikali imelazimika kuzitoza kodi taasisi za dini kutokana na baadhi kufanya kazi katika mazingira ya kibiashara badala ya huduma.

Alitoa kauli hiyo jana mkoani Morogoro alipofungua Mkutano Mkuu wa 31 wa Jumuiya ya Kikristu Tanzania (CCT) ambao moja ya ajenda zake ni uchaguzi wa viongozi.

Akijibu ombi la jumuiya hiyo kuhusu kuondoa kodi kwa taasisi za kidini zinazotoa huduma ya afya na elimu, Rais Samia alisema suala hilo pia liliwasilishwa kwake na Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC) na anaamini akienda Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) nao watamweleza hayo hayo.

"Wakati mwingine serikali inalazimika kuzitoza kodi taasisi za kidini za elimu na afya kwa sababu baadhi zina mazingira ya kufanya kazi kibiashara na siyo huduma.

"Hapa ndipo unapokuja ushindani wa huduma kati ya taasisi ya dini na serikali, unakuta huduma hapa na serikali nayo inajenga kituo cha afya hapo, wananchi wakienda kupata huduma huko wanatoa fedha nyingi kuliko serikalini," alifafanua.

Alisema suluhisho la tatizo hilo ni wote wafanye kazi kwa uwazi na kuaminiana ili watoza kodi wajue kwamba taasisi za dini hazifanyi biashara.

Alikiri kumetokea shida mbili au tatu katika mifumo hiyo, shule ambazo zinatoa huduma ya elimu na afya kwa Watanzania kwa msaada kutoka nje lakini bado taasisi za kodi zinakwenda kuzitoza kodi.

"Ukilitizama unaona hakuna mantiki, wamekusanya jasho la wengine. Wanatoza kodi kwa sababu hakukuwa na uwazi katika kufanya kazi. Niziombe taasisi hizi zifanye kazi kwa uwazi na kuaminiana," alisema.

Rais Samia alisema mbali na taasisi za dini, huduma hizo pia zinatolewa na sekta binafsi na wakitazama malipo ya ada na huduma zinazotolewa zikiwamo afya, wanakuta mambo ni yale yale ndiyo maana kukawa na mwonekano wa taasisi za dini kufanya biashara.

Alisema endapo wataondoa kodi kwa taasisi za dini ambazo utendaji wake unaendana na ule wa sekta binafsi kutakuwa hakuna uwanja sawa wa kufanya shughuli hizo.

**MAPITIO YA KODI**

Rais Samia alisema serikali imeanza kupitia kodi na kuzifuta baadhi yake, akitolea mfano tozo ya elimu, mafunzo ya ufundi stadi (SDL) iliyolalamikiwa kwa muda mrefu.

Rais Samia alisema wakimaliza kazi hiyo ana uhakika mambo mengi ambayo taasisi za dini zinayalalamikia yatakuwa yamepata ufumbuzi.

**VIBALI VYA KAZI**

Kuhusu suala la upatikanaji wa vibali vya kazi na vya kuishi kwa wataalamu wa kujitolea kutoka nje katika sekta ya elimu na afya, Rais Samia alisema limeshafanyiwa kazi tangu Aprili 23, mwaka huu na sasa vinatolewa kupitia mfumo wa kielektroniki unaopunguza urasimu na mazingira ya rushwa.

**SIASA NA DINI**

Rais Samia alisema wakati mwingine dini na siasa ni vitu vinavyokwenda sambamba lakini hukinzana kwa kutegemea mtu anazitumiaje.

"Siyo vibaya kiongozi wa dini kuwa mwanasiasa lakini kuna ubaya anapotumia dini kufanya siasa, yote inabidi tuyatazame kwa umakini," alifafanua.

**UTAWALA KISHERIA**

Rais Samia pia aliishukuru CCT kwa kuunga mkono serikali katika suala ambalo inalitekeleza la kuheshimu utawala wa sheria na haki za binadamu na kueleza kuwa hawatasita kuchukua hatua kwa viongozi au watendaji serikalini wasioheshimu hilo.

"Niendelee kuwahimiza viongozi wa dini zote kuwahimiza wananchi kuheshimu utawala wa sheria na taratibu za nchi, msisite kuwakemea wanaovunja sheria kwa makusudi na kuhatarisha amani," alisema.

Vilevile, Rais Samia alitumia mkutano huo kuwaomba viongozi wa dini kuwakumbusha waumini umuhimu wa kujikinga na kuchukua tahadhari dhidi ya corona na kuliombea taifa na dunia ili Mungu aliepushe.

**•Imeandaliwa na Romana Mallya (DAR) na Christina Haule (MORO)**

# Ndalichako aagiza vyuo, shule kuzingatia mwongozo wa corona

**Na Gwamaka Alipipi**

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, amevitaka vyuo vikuu, shule za msingi na sekondari kuhakikisha vinazingatia mwongozo wa udhibiti wa maambukizi ya COVID-19 uliotolewa, kabla ugonjwa huo haujasababisha madhara makubwa nchini.

Amesema hatarajii kuchukua uamuzi wa kufunga shule, vyuo wakati uwezo wa kuudhibiti ugonjwa huo upo.

Ndalichako alitoa agizo hilo jana jijini Dar es Salaam wakati akikabidhi vifaa vya mafunzo ya utengenezaji wa ndege kwa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), vyenye thamani ya Sh. milioni 245.466. "Nitumie nafasi hii kuzitaka taasisi za elimu nchini kuzingatia mwongozo uliotolewa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto wa kukabiliana na ugonjwa wa corona, kabla hali haijawa mbaya.

Julai 4, mwaka huu, serikali ilifanya maboresho ya mwongozo wa udhibiti wa maambukizi ya COVID-19, katika shule, vyuo na taasisi za elimu ili ukidhi mahitaji ya sasa ya kuwakinga wanafunzi na maambukizi ya virusi vya corona. Kuhusu kukabidhi vifaa vya uhandisi wa ndege, Prof. Ndalichako alisema vitaiongezea NIT ufanisi wa ufundishaji pamoja na kutimiza malengo iliyojiwekea na ya kitaifa.

Mkuu wa NIT, Prof. Zacharia Mganilwa, alisema programu ya mafunzo ya uhandisi wa ndege ilianzishwa mwaka 2015 na hadi sasa imeshatoa wahitimu 75, kati yao 26 ni wahitimu wa stashahada, 49 ni wa shahada ya kwanza.

"Asilimia 60 ya marubani waliopo hapa nchini ni raia wa kigeni. Wahandisi wa ndege wengi wanatoka nje ya nchi. Gharama ya kusoma uhandisi wa ndege nje ya nchi ni Sh. milioni 200 hadi 300 kwa mtu mmoja," alisema Prof. Mganilwa. Alisema kwa hapa nchini, gharama ya kusoma uhandisi wa ndege ni Sh. milioni sita, kuiomba serikali kutoa ruzuku kwa wanafunzi wanaohitaji kusoma fani hiyo ili kuongeza idadi.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), Bahati Geuzye, alisema: "Fedha za ununuzi wa vifaa umetolewa na Wizara ya Elimu kupitia Mamlaka ya Elimu Tanzania, kwamba ufadhili huu utasaidia NIT kuimarisha masomo ya usafiri wa anga, matengenezo ya ndege, vijana wengi watafikia malengo yao."

HABARI KITAIFA

# Aliyefungwa miaka 30 afutiwa kifungo

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Musoma, imemfutia adhabu ya kifungo cha miaka 30 jela na kumuru atolewe gerezani, Kabambe Musyome, aliyekuwa anatumikia kifungo hicho baada ya kutiwa hatiani kwa kosa la unyang'anyi wa kutumia silaha.

Uamuzi wa Mahakama hiyo ulitolewa mbele ya Jaji Edson Mkasimongwa, aliyesikiliza rufani hiyo ya kupinga adhabu ya kifungo cha miaka 30 jela na kupitia ushahidi wa pande zote mbili.

"Katika kesi hii Anna Nyantori, anayedaiwa kuvamiwa na kujeruhiwa alishindwa kumtambua aliyemvamia sababu tukio lilitokea usiku.

"Rufani imekubaliwa, adhabu dhidi ya mrufani inafutwa, mahakama inaamuru aachiwe mara moja gerezani kama hana kesi nyingine inayosababisha aendelee kuwa huko," alisema Jaji Mkasimongwa.

Kabambe alitiwa hatiani na kuhukumiwa kifungo cha miaka 30 jela na kulipa fidia ya Sh. 200,000 na Mahakama ya Wilaya ya Serengeti.

Inadaiwa Machi 27, 2019 kati ya saa nne na tano usiku, Nyantori ambaye ni mfanyabiashara alikuwa akirudi nyumbani maeneo ya Sedeco Mugumu.

Nyantori alikuwa akiendeshwa na David Mahende, walipofika Stendi Mpya akiwa ndani ya gari alivamiwa na watu wawili wakamtoa Nyantori ndani ya gari.

Wavamizi hao walikuwa na chuma wakamjeruhi maeneo ya miguu na mdomoni, Mahende alijeruhiwa mkono wa kushoto na kufanikiwa kuiba simu mbili pamoja Sh. 100,000.

Mahakama Kuu wakati inafikia uamuzi ilihoji maswali kwamba je, uvamizi ulikuwa wakutumia silaha? Na je, mvamizi alikuwa mmoja na wengine?

Alisema hoja ya mrufani kwamba Nyantori alishindwa kumtambua aliyemvamia sababu ilikuwa usiku ni muhimu kwa mahakama kuipima.

Katika sababu za rufani, Kabambe anasema Mahakama haikumtendea haki kumtia hatiani na kumpa adhabu ya kifungo cha miaka 30 jela wakati aliyevamiwa alishindwa kumtambua kwamba mrufani ndiye aliyetenda tukio hilo.

Shahidi namba mbili na tatu walishindwa kutambua nani alihusika katika tukio hilo, upande wa Jamhuri ulishindwa kuthibitisha mashtaka bila kuacha shaka na Mahakama ilishindwa kupima na kuhakiki maelezo na ushahidi wa mrufani dhidi ya mashtaka yaliyokuwa yakimkabili.

Katika hoja hizo mahakama ilikubaliana na hoja kwamba Nyantori anayedaiwa kuvamiwa alishindwa kutambua nani aliyehusika katika tukio hilo sababu ilikuwa usiku, kiza na hakuna maelezo kwamba kulikuwa na taa eneo hilo.

Rufani ilikubaliwa, mrufani aliachiwa na alifutiwa adhabu na Mahakama kuamuru atolewe gerezani. Katika rufani hiyo mrufani alikuwa akijiwakilisha mwenyewe na Jamhuri iliwakilishwa na Wakili wa Serikali, Nimrod Byamungu.




Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela (kulia), akitambulishwa na Mkurugenzi wa Rasilimali Watu wa Benki ya CRDB, Siaphoro Kishimbo, kwa wanafunzi wa vyuo vikuu ambao wamechaguliwa kushiriki programu ya mafunzo ya uongozi kwa wahitimu wa vyuo vikuu "Graduate Development" inayoendeshwa na benki hiyo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri aagiza watumishi wasimamishwe tuhuma za ubadhirifu fedha za hospitali

**Na Mwandishi Wetu,** IRINGA

NAIBU Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mwanaidi Ali Khamis, ameagiza kusimamishwa kazi kwa watumishi watatu wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Iringa kwa tuhuma za ubadhirifu.

Watumishi hao wanadaiwa kushirikiana na mawakala wa benki kuchepusha takribani Sh. milioni 20 kwa ajili ya ununuzi wa dawa hospitalini hapo.

Alitoa agizo hilo katika kikao na watendaji waandamizi wa hospitali hiyo ikiwa ni sehemu ya ziara yake mkoani Iringa.

Alipata taarifa kutoka vyanzo maalum kuwa baadhi ya watumishi wanashirikiana na mawakala wa benki kuchepusha fedha za hospitali kwenda kwenye akaunti zao binafsi.

"Nimesikia taarifa ya hospitali lakini nahoji sikusikia taarifa za upotevu wa fedha za hospitali kupitia akaunti za watumishi wa hapa au siyo hospitali hii?" Alihoji Niabu Waziri.

Alisema serikali inatoa fedha nyingi kwa ajili ya ununuzi wa dawa katika hospitali, hivyo akiwa msaidizi wa Rais katika sekta husika, hatafumbia macho vitendo vyovyote vya ubadhirifu wa fedha za umma.

Pia aliuagiza uongozi wa hospitali hiyo kusimamia kwa ukamilifu matumizi ya fedha zinazoletwa na serikali kwa malengo ya kutoa huduma kwa wananchi na si kujinufaisha watu wachache.

"Niseme hatuwezi kuvumilia haya madudu kabisa. Fedha zinatolewa na serikali kuja kutoa huduma kwa wananchi, lakini wewe mtumishi wa umma unajimilikisha. Hili hapana tunashughulika nalo," alisema.

Katibu wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Iringa, Abbas Idd, amesema ni kweli tukio hilo limetokea na linafanyiwa kazi na vyombo vya uchunguzi ili kubaini wale wote waliohusika na kuwachukulia hatua.

"Mheshimiwa Naibu Waziri kulikuwa na matukio mawili tofauti lakini kama ni suala hilo, kweli kuna baadhi ya wafanyakazi wenzetu wamebainika kushirikiana na baadhi ya mawakala wa benki na kuhamisha fedha za malipo ya dawa kwenda kwenye akaunti zao binafsi," alisema Abbas.

Baada ya maelezo hayo, Naibu Waziri aliagiza kudhibitiwa kwa akaunti za watumishi na mawakala wa benki waliohusika na kuhakikisha uchunguzi wa kina unafanyika ili kuepusha udanganyifu wa aina hiyo kuendelea kutokea.

Pia aliwataka mawakala wa benki walioshirikiana na watumishi wa hospitali hiyo kuchepusha fedha za umma, kuzirejesha ili kufidia hasara iliyopatikana.

# Kalemani azindua ulipaji wa fidia bomba la mafuta

**Hafsa Omar,** TABORA

WAZIRI wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, amezindua rasmi ulipaji wa fidia kwa wananchi walioopisha mradi wa ujenzi wa bomba la kusafirisha mafuta ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Akizungumza katika hafla hiyo iliyofanyika juzi katika kijiji cha Sojo, Nzega, mkoani Tabora, Dk. Kalemani alsiema kazi hiyo imeanza rasmi na watu wote watafidiwa kwa usahihi na kwa wakati.

Pia alisema gharama za fidia katika mradi mzima kutoka Kyaka mkoani kagera hadi Chongoleani, Tanga ni Sh. bilioni 28.26.

Alisema serikali imeamua kuzindua ulipaji wa fidia katika kijiji cha Sojo kwa sababu eneo hilo liko katikati baina ya Hoima nchini Uganda na Chongeleani, Tanga na kuwataka wasimamizi wa mradi huo kujenga karakana katika eneo hilo kwa kuwa karakana zinajengwa katikati ya mradi.

Kwa mujibu wa Kalemani, wanufaika wa mradi huo watakuwa Watanzania wote kwa jumla lakini waliopitiwa na mradi watanufaika zaidi kwa sababu fursa mbalimbali zitapatikana wakati wa ujenzi wa mradi na kuwataka wananchi kujitokeza kuchukua fursa mbalimbali za mradi.

Pia alisema eneo hilo ndio linatumika kujenga kambi, hivyo wananchi wa sehemu hiyo watafaidika na ujenzi wa huduma za kijamii kama vile kituo cha afya, shule na barabara ambazo zitajengwa baada ya ujenzi wa mradi kuanza.

Dk. Kalemani aliwataka wananchi ambao watalipwa fidia zao kuanza kuondoka kwenye maeneo hayo ili ujenzi wa mradi uanze mara moja.

"Ukishalipwa na pesa umepewa na ni haki yako, basi pisha mradi asije akatokea mtu akalipwa halafu akazitumia pesa zote baadaye akasema pesa alizolipwa ni ndogo. Kwa hiyo tuheshimu malipo ya fidia na tuzitumie pesa kwaajili ya maendeleo," alisema.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Dk. James Mataragio, aliosema ulipaji fidia utaanza kwa maeneo yote 12 na timu za wawakilishi wa serikali, Kampuni ya EACOP, Kampuni ya Uthamini (White Night) na Kampuni ya Ushirikishaji na Kusaidia Jamii (JSB) ziko katika baadhi ya mikoa kwa utekelezaji wa kazi hiyo.

alisema baada ya kukamilika kwa taratibu, wananchi 391 waliopisha mradi watalipwa fidia na kwamba kati ya hao 44 wametoka kijiji cha Sojo ambao baadhi yao walitia saini mikataba ya kulipwa.

# Ndugulile apongeza huduma mpya TTCL

Na Mwandishi Wetu

WAZIRI wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Faustine Ndugulile, amelipongeza Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL) kwa kuja na bidhaa za ubunifu, zikiwamo zinazojibu kero zilizotokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Dk. Ndugulile alitoa pongezi hizo jana kwenye banda la TTCL kwenye Maonyesho ya Kimataifa ya Biashara ya 45 yanayoendelea Viwanja vya Sabasaba, Dar es Salaam, alipotembelea kujionea bidhaa na huduma mbalimbali zinazotolewa na TTCL.

Alisema TTCL na Kituo cha Taifa cha Intaneti (NIDC) wamekuja na mfumo wa ukusanyaji wa fedha katika baadhi ya mageti na huduma kwa kutumia kadi za kitaifa za kutunzia fedha na kufanya miamala inayojulikana kama 'N-Card' inayofanya kazi katika Kivuko cha Feri Kigamboni na kwenye viingilio vya mchezo wa mpira wa miguu kwa baadhi ya viwanja.

Alisema TTCL pia imeleta huduma ya kufanya mikutano kwa njia ya video 'video conference', huduma ambayo inawawezesha watu kufanya mikutano yao bila kurundikana eneo moja.

Alisema matumizi ya 'N-Card' yanaondoa utaratibu wa awali wa malipo ya fedha taslimu kwa kulipa papo hapo hususan katika maeneo yenye misongamano wa malipo kama katika viingilio uwanjani, baadhi ya mageti na hata kwenye matamasha utaratibu ambao ni hatari.

Meneja wa Banda la TTCL, Ramadhani Mshana, akizungumza ndani ya banda lao alizitaka taasisi binafsi na za umma zinazohitaji kupatiwa huduma mpya za 'call center' kutembelea banda la TTCL kupata suluhisho hilo pamoja na huduma zingine ikiwamo mikutano ya mtandaoni.

Alibainisha bidhaa na huduma zingine zinazopatikana ndani ya banda lao ni pamoja na vifaa vya intaneti kama MiFi, Router, Dongle, Wingle na simu za mezani.

Aliongeza kuwa huduma zingine zinazotolewa ndani ya banda la TTCL, ni pamoja na kutoa bure laini za simu kwa wateja.

# Jenista aibana NDC kuilipa NSSF mkopo bil. 4.5/-

Na Mwandishi Wetu

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, ametembelea kiwanda cha viuadudu kilichopo Kibaha mkoani Pwani na kuliagiza Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC), kulipa mkopo wa Sh. bilioni 4.5 walizokopa katika Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF).

Alitoa agizo hilo jana, alipotembelea kiwanda hicho kwa ajili ya kujionea shughuli zinazofanywa na kusema mwaka 2016, NSSF iliikopesha NDC kiasi hicho cha fedha, lakini kwa sababu mkopo umelipwa kiasi kidogo sasa umefikia karibu Sh. bilioni nane.

"Fedha hizi ni za wanachama, kazi ya mfuko ni kuandikisha wanachama kutoka sekta binafsi na isiyo rasmi, kukusanya michango, kuwekeza na kulipa mafao, hivyo NDC ndio wadau waliokopa kwa hiyo wahakikishe wanarudisha mkopo huu kwa sababu ni fedha za wanachama wetu," alisema.

Waziri Jenista alisema tayari kamati imeundwa ili kuja na mapendekezo kwa ajili ya kuokoa kiwanda hicho, na ameongea na Waziri wa Viwanda na Biashara, Profe. Kitila Mkumbo, ili kamati hiyo kama haijaanza kazi iweze kuanza mara moja na kuhakikisha fedha za NSSF zinarudishwa.

Alisema amewaagiza NSSF mkopo huo ulipwe na fedha za wanachama zirudishwe kama zilivyowekwa kwa utaratibu ambao unawezekana ili fedha hizo zibaki katika utaratibu wa kulipa mafao muda unapofika.

"Tumekuwa tukishauriwa NSSF wasiwekeze wenyewe, wasiendeshe viwanda wenyewe, lakini waangalie wanaweza kuingia ubia na nani, na katika kiwanda hiki wapo ubia na NDC ambao tunawakumbusha fedha hiyo wailipe kwani tunaitaka iende kwenye mfuko ikafanye kazi tulizokusudia," alisema. Jenista alisema NDC ni taasisi ya serikali kwa hiyo inawajibu wa kuzungumza ndani ili kuondoa vikwazo na kuhakikisha kiwanda kinaendelea kukua kama matarajio yalivyokubaliwa kutokana na kiwanda hicho kuwa muhimu kwa maendeleo ya taifa.

Akizungumzia kero za wafanyakazi wa kiwanda hicho, Waziri Jenista alisema wamekubaliana na Wizara ya Viwanda na Biashara, iingilie kati ili kumaliza changamoto zilizopo.

Alisema suala jingine ni la masoko kutokana na baadhi ya nchi za SADC na za Afrika Mashariki kuanza kuchangamkia dawa zinazotengenezwa kiwandani hapo, na kuiagiza NDC kukitangaza kiwanda hicho.

Naye Mkurugenzi wa Uwekezaji wa NSSF, Gabriel Silayo, alisema Mfuko uliwekeza takribani Sh. bilioni 4.5 fedha ambazo walizikopesha kwa NDC, na kwamba wamepokea maagizo ya Waziri Jenista na kuahidi kukaa na NDC ili mkopo huo uweze kulipika kwa maslahi ya wanachama na mfuko kwa ujumla.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, akiangalia darubini alipotembelea kiwanda cha viuadudu, kilichopo Kibaha mkoani Pwani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Vikwazo 30 vya biashara na Kenya kutatuliwa Agosti

Na Joseph Mwendapole

KENYA imesema vikwazo 30 vya biashara kati ya nchi yake na Tanzania vitapata ufumbuzi ifikapo mwezi ujao.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Balozi wa Kenya nchini, Dan Kazungu, wakati akizungumza na ujumbe wa wafanyabiashara wa Shirikisho la Wenye Viwanda Kenya (KAM) na Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania (CTI).

Alisema mawaziri wa Kenya na Tanzania wamefanikiwa kuondoa vikwazo 34 ambavyo vimekuwa mwiba kwa biashara mipakani yakiwa ni matunda ya ziara ya Rais Samia Suluhu Hassan nchini humo hivi karibuni.

Alisema mawaziri hao walikutana hivi karibuni jijini Arusha kujadili vikwazo 64 vya biashara ambapo ndani ya siku nne pekee walifanikiwa kuondoa vikwazo 34 vya biashara mipakani.

"Vikwazo 30 vilivyobaki nawahakikishia kwamba mwezi wa nane hautapita kabla havijaondolewa kwa hiyo kazi kwenu wafanyabiashara kwa sababu hakutakuwa tena na vikwazo, fanyeni biashara sisi ni ndugu moja hatupaswi kuwekeana vikwazo," alisema Balozi Kazungu.

Alisema nchi za Afrika Mashariki ni soko kubwa ambalo watu wengi wanalitamani hivyo, kuna umuhimu wa nchi hizo kuondoa vikwazo ili biashara zishamiri na kuchangia kwenye ukuaji wa uchumi kwenye nchi hizo na kuongeza ajira kwa watu wake.

"Sisi ni ndugu kabisa na hata kiongozi akiamua tu kuweka vikwazo ili kuwatenganisha Wakenya na Watanzania kwa sababu tu ana cheo cha kufanya hivyo mwishowe atakuta tunakaa na kuzungumza kwa sababu undugu wetu hauwezi kutenganishwa na mtu yeyote," alisema.

Aliwaambia wafanyabiashara hao kuwa mambo mengi makubwa na mazuri yanakuja, kwani marais wa nchi hizo mbili wamefungua milango ya ushirikiano wa kibiashara hivyo waitumie fursa hiyo ipasavyo ili kuneemesha biashara zao.

Alisema ziara ya Samia ilikuwa na manufaa makubwa na ndiyo imesababisha wafanyabiashara kutoka Kenya kuja nchini kukutana na wazalishaji wenzao kubadilishana mawazo namna bora kushirikiana.

"Ziara ya Rais Samia nchini Kenya ilitupa heshima sana, iliwafurahisha Wakenya wengi kwa sababu ilikuwa ziara yake ya kwanza na kuna nchi nyingi ambazo angeweza kwenda, lakini hatua ya kuichagua Kenya kwetu sisi ilikuwa ni heshima kubwa sana," alisema.

Mwenyekiti wa CTI, Paul Makanza, alisema wafanyabiashara wa Tanzania wakiongozwa na shirikisho hilo watakwenda nchini humo kama sehemu ya kuimarisha uhusiano na wafanyabiashara wa nchi hiyo.

Makanza alisema nchi za Afrika Mashariki zina fursa muhimu na kubwa kibiashara kutokana na idadi kubwa ya watu waliomo hivyo ushirikiano wa kibiashara kati ya wafanyabiashara hao ni jambo ambalo haliepukiki kwa ustawi wa mataifa hayo.

Mwenyekiti wa Shirikisho la Wafanyabiashara wa Kenya, Mucai Kunyiha, alisema ushirikiano kati ya KAM na CTI ni wa muda mrefu, hivyo ujio wa ujumbe kutoka Kenya ni kwa ajili ya kuimarisha na kuuendeleza.

Alisema sekta binafsi ni muhimu kwenye ukuaji wa uchumi, hivyo wanakutaka kujadiliana namna ya kutimiza wajibu wao ili kusaidia nchi hizo kufanya vizuri kiuchumi na namna ya kuzungumza na serikali zinapotokea changamoto za kibiashara.

"Kwetu Kenya tukiwa na tatizo huwa tunazungumza na serikali, na kwa kweli huwa wanatusikiliza na kutatua vikwazo vya kibiashara... sasa hiyo hali inapaswa iwe kwenye nchi zote za EAC mazingira ya biashara yawe rahisi," alisema Kunyiha.

# Muhimbili ilivyohudumia wananchi wengi Sabasaba

**Na Christina Mwakangale**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH), imesema kati ya wananchi 2,000 waliotembelea banda la hospitali hiyo kwenye Maonyesho ya Sabasaba, 921 walifanyiwa uchunguzi na tiba.

Aidha, kati yao 13 waliopatiwa huduma mbalimbali kutoka kwa mabingwa wa MNH, walipewa rufani kufika hospitalini kwa ajili ya tiba na uchunguzi zaidi.

Takwimu hizo ni kwa mujibu wa Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano kwa Umma MNH, Aminiel Aligaesha, kuhusu idadi ya waliotembelea banda lao kuanzia Juni 28 hadi Julai 3, mwaka huu kwenye Maonyesho ya 45 Biashara Kimataifa ya Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa takwimu hizo, kati ya 921 waliopatiwa huduma kati yao 333 walihudumiwa magonjwa ya macho, 180 huduma za lishe na 58 magonjwa yaliyohusiana na ngozi.

Pia 194 walihudumiwa kitengo cha magonjwa ya dharura, huku 143 wakipewa huduma ya afya ya kinywa, na kwamba takwimu hizo ni kwa kipindi cha takribani wiki moja tangu kuanza kwa maonyesho hayo.

Aidha, alisema takwimu kuhusu huduma za MNH kwenye maonyesho hayo zitatolewa tena, Julai 13, mwaka huu ikiwa ni tathmini ya huduma kwa wananchi viwanja vya Sabasaba.

Pia, jamii imetakiwa kujenga mazoea ya kupima afya ili kuzuia magonjwa ya macho kama vile, shinikizo la jicho, uono hafifu na wakati mwingine upofu.

Wataalamu wa afya walishauri jamii kupima macho kwa sababu watu wengi wana matatizo makubwa ya macho kutokana na kuchelewa kwenda hospitali.

Mtaalamu wa macho wa MNH, Dk. Neema Moshi, alisema magonjwa ya macho yapo ambayo yanaonyesha dalili na mengine hayaonyeshi katika hatua za awali.

"Yapo magonjwa ya macho yanayokuja na uvimbe, maambukizi na wakati mwingine mtu anapoteza uono kwa haraka, lakini magonjwa ya macho mengine hayana dalili katika hatua za awali kama shinikizo la jicho na uharibifu wa jicho kutokana na magonjwa kama kisukari, shinikizo la damu, selimundu na Ukimwi," alifafanua Dk. Neema.

Dk. Yusta Mtogo kutoka Hospitali ya Muhimbili-Mloganzila, alitoa wito kwa jamii kupima afya mara kwa mara, na kwamba magonjwa mengi ya macho yanasababisha upofu unaozuilika.

# Kunenge awaangukia viongozi dini ubakaji, dawa za kulevya

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge (pichani), amewaomba viongozi wa dini wawapo kwenye nyumba za ibada kukemea ubakaji, uvamizi wa maeneo, wizi na matumizi ya dawa za kulevya.

Kunenge aliyasema hayo jana alipokutana na viongozi wa dini kutoka katika maeneo mbalimbali ya mkoa huo, kwa lengo la kujitambulisha kwao.

Alisema viongozi wa dini wana nafasi ya kukemea vitendo hivyo kwenye nyumba za ibada, eneo ambalo ndilo wanapokutana na wananchi wengi kwenye ibada.

"Nilipokuwa nazunguka huko kwenye wilaya, nimekuwa nikiwaomba wanaofanya vitendo hivi waache...sasa muda wa kutoa rai na kuomba umekwisha, mnisaidie kukemea tutakapoanza kuchukua sheria tusilaumiwe," alisema.

Kunenge alisema hakuna eneo serikali inashindwa kulifanyia kazi, hivyo hatua zikianza kuchukuliwa hakuna kurudi nyuma na hakutakuwa na yeyote atakayeonewa.

Alisema katika migogoro ya ardhi sheria ifuatwe, kwani hadi sasa ana taarifa za migogoro ya ardhi zaidi ya 200, ambayo itaanza kushughulikiwa kwa ushirikiano na Waziri wa Ardhi.

Kunenge alitumia nafasi kuruhusu mikutano ya dini, huku akisisitiza kuzingatia sheria na taratibu za vibali vya mikutano wanayoomba.



Mwenyekiti Mwenza wa Kamati ya Amani, Hamis Mtupa, alisema wanatarajia kuandaa kongamano la viongozi wa dini kushirikiana na Jeshi la Polisi kuhusiana na mikakati ya kukomesha ubakaji katika mkoa huo.

Mmoja wa viongozi wa dini aliyeshiriki kikao hicho, Mohamed Tundiya, aliomba kamati za ulinzi na usalama za kata kufanya kazi zao ipasavyo kabla matatizo hayajakomaa na kuleta athari kubwa.

Naye Jauna Sembo, alimwomba Mkuu wa Mkoa kushughulikia suala la mapori katika kata ya Sofu, ambayo yamekuwa maficho ya wezi na wadudu wakali.

TRA

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU TRA KUKUTANA NA WADAU WA FILAMU NCHINI**

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), itakutana na wadau wa Filamu nchini siku ya **tarehe 10 Julai, 2021** kwa ajili ya kujadili kodi mbalimbali zinazogusa mazao ya filamu ikiwemo Kodi ya Zuio (Withholding Tax) na Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT).

Katika kikao hicho, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) itakuwepo kutoa ufafanuzi juu ya sera ya matangazo ya biashara kwenye chaneli za kulipia (Pay TV).

Aidha, Bodi ya Filamu Tanzania ikiwa ni Taasisi inayosimamia Sekta ya Filamu na Michezo ya Kuigiza nchini itahudhuria kama mlezi wa tasnia hiyo.

Kikao hicho kitafanyika katika ukumbi wa Chuo cha Kodi (ITA)
**P.O.Box 9321, Mikocheni Dar es salaam Tel: +255 22 2216800/1**
au **+255 783081348 Email: ita@tra.go.tz kuanzia saa 7:00 mchana.**

Wadau wote wa filamu nchini wanakaribishwa.

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

Imetolewa na;
**KAMISHNA WA KODI ZA NDANI**

216349502

**MAONI & UCHAMBUZI**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Riba za benki kilio cha muda mrefu, tuone marekebisho sasa

**KILIO** cha riba kubwa za mikopo inayotolewa na benki nchini ni cha muda mrefu kiasi cha wengi kushindwa kukopa, na kila kiongozi wa nchi aliyeingia madarakani aliliongelea na kuzitaka taasisi hizo kupunguza ili kuwezesha wananchi kukopa kwa ajili ya kutekeleza shughuli za maendeleo.

Kwa mara ya kwanza Rais wa Awamu ya Nne Jakaya Kikwete kipindi cha utawala wake alizungumzia suala hilo na kuzitaka benki kuangalia uwezekano wa kupunguza riba hizo ili kuwezesha watu wengi zaidi kukopa kwa ajili ya uwekezaji na maendeleo kwa ujumla.

Mafanikio yalikuwapo lakini ni kidogo sana na riba zilitofautiana kati ya benki moja hadi nyingine kwa kuwa wapo walitoza hadi asilimia 22 na wengine asilimia 18, ambazo bado ziliendelea kuwa mzigo mzito kwa mkopaji.

Alipoingia Rais wa Awamu ya Tano, Hayati John Magufuli, alizungumzia suala hilo na mwaka 2018 Benki Kuu ya Tanzania (BoT), ilipunguza riba ya kukopesha benki kutoka asilimia 16 hadi tisa, na iliahidi kushusha zaidi ili kuzifanya taasisi hizo kushusha riba na kuwezesha wananchi wengi wenye sifa kukopa kwa ajili ya shughuli za maendeleo.

Juzi Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mhandisi Hamad Yussuf Masauni, aliagiza BoT kutekeleza haraka maelekezo yaliyotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan, ya taasisi za fedha nchini kupunguza riba za mikopo.

Pia Naibu Gavana wa BoT, Dk. Bernard Kibesse, alimhakikishia waziri huyo kwamba wanakamilisha mazungumzo na benki washushe riba kama alivyoelekeza Rais Samia jijini Mwanza mwezi uliopita alivyozungumza na vijana.

Alikwenda mbali zaidi na kusema kuwa BoT inaendelea kurekebisha kanuni mbalimbali za mikopo inayotolewa na BoT kwa benki ili kuziongezea ukwasi na zenyewe zitumie fursa hiyo kushusha riba za mikopo.

Ikiwa jambo hili litatekelezwa ni wazi kuwa kutakuwa na manufaa kwa wananchi, taasisi za fedha na taifa kwa ujumla, kwa kuwa watakaochukua mikopo watawekeza na kuajiri, kuchangia GDP na kodi mbalimbali, lakini maendeleo yatazidi kustawi kutokana na shughuli za kiuchumi.

Pia benki zitaendelea kupata wateja wengi na faida, lakini serikali itaongeza idadi ya walipa kodi wakubwa, wa kati na wadogo, pia itapata kodi kutokana na shughuli za kiuchumi.

Kutokana na riba za benki kuwa juu wengi wamekimbilia kwenye vikundi kupata mikopo midogo, na baadhi Vyama vya Akiba na Mikopo (SACCOS), ni muhimu riba hizi zikashuka kwa kuwa tunajua benki ndiyo zinaweza kutoa mikopo mikubwa kuanzia Sh. milioni 20 kuendelea.

Ikiwa riba zitakuwa rafiki maana yake wafanyabiashara na wawekezaji wa ndani watakopa kwenye benki zetu na kuwekeza kwenye miradi au shughuli ambazo zitaajiri watu wengi, na kupunguza tatizo la ajira nchini ambalo linakuwa kwa kasi. Ni wazi kuwa serikali haiwezi kuajiri kila Mtanzania bali kazi hiyo inafanywa pia na sekta binafsi ambayo ni injini ya ukuaji uchumi wa nchi yoyote duniani, na ndiyo imeajiri mamilioni ya watu na ili izidi kuchanua ni lazima kuiongezea nguvu kwa kupunguza riba za mikopo.

Wakati wa utawala wa Rais Kikwete alitambua umuhimu wa sekta binafsi na ndiyo maana alihakikisha anakuwa imara, kiasi cha kuajiri watu wengi na siyo kila mtu kukimbilia ajira za serikalini ambazo ni chache.

Ni matarajio yetu ahadi ya BoT itatekelezwa kwa vitendo na siku za hivi karibuni tunashuhudia benki zikitoza riba ndogo ambayo haitawaumiza wao wala wakopaji, na hilo litawezekana iwapo mamlaka ya usimamizi itawajibika kwa kufanya marekebisho ya kanuni zake.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com





Na Rajabu Msangi, SJMC

**Muungwana Lazima Nilonge**

# Tahadhari zinahitajika kuendelea kuepuka janga corona nchini

**BADO** kuna tafakuri kwa wananchi na hakuna anayejua kina kirefu cha tafakuri hiyo katika hoja ya ugonjwa wa corona utaondoka lini duniani.

Hivi sasa, Bara la Afrika na nchi zake zinakabiliwa na wimbi la tatu la maambukizi ya virusi vya corona. Tanzania nasi tumeingia katika orodha.

Baadhi ya nchi za Afrika zimechukua tahadhari za tofauti ikiwamo, majirani Uganda wanaotangaza kufungwa shule zote kwa siku 42, kutokana na ongezeko la maambukizi ya virusi vya corona nchini humo.

Kwa Tanzania, Machi 16 mwaka jana, mgonjwa wa kwanza aliripotiwa kupata virusi vya corona mkoani Arusha, ikiwa muda mfupi baada ya kutua kwenye Uwanja wa Kimataifa wa Kilimanjaro, akitokea ughaibuni.

Hilo liliweka hofu kubwa kwa Watanzania. Ingawaje virusi hivi vilianzia huko Wuhan, nchini China mwaka 2019, hatimaye kuanza kusambaa katika nchi mbalimbali duniani.

Kutoka katika wimbi la kwanza la virusi hivi hadi kufikia katika wimbi la tatu, kunazidi kushangaza jamii kwa kuwa virusi hivi bado havijatokomea kabisa. Ni raia wengi wamepoteza maisha kufuatia janga hili na wengine kuambukizwa maradhi haya.

Ni rasmi ugonjwa huo, awamu ya tatu umeshaingia nchini na Rais Samia Suluhu Hassan, alianza kuiweka wazi alipozungumza na wenyeji wake, katika ukumbi wa Baraza la Maaskofu Tanzania (TEC), jijini Dar es Salaam.

"Tumetoka kwenye wimbi la kwanza Tanzania tumeingia, limekwenda limepungua kidogo limeingia la pili na sasa tuna wimbi la tatu. Ishara ndani ya nchi zinaonekana tayari tuna wagonjwa ambao wameshaonekana katika wimbi hili la tatu," alitamka.

> **"Tumetoka kwenye wimbi la kwanza Tanzania tumeingia, limekwenda limepungua kidogo limeingia la pili na sasa tuna wimbi la tatu. Ishara ndani ya nchi zinaonekana tayari tuna wagonjwa ambao wameshaonekana katika wimbi hili la tatu,"**

Katika hatua hiyo, pia alitumia fursa pana kuwataka Watanzania kupitia viongozi wa dini, waendelee kuchukua tahadhari dhidi ya kupambana na janga hilo la maradhi, kupunguza vifo vya umma.

Rais alitamka, kinga ni bora kuliko tiba, tusiache kutumia kila kitakachotukinga na maradhi haya ili kuepusha vifo vya makundi.

Rais Samia, pia alisema hadi sasa kuna idadi ya wagonjwa 100 ambapo kati yao 70 wanapatiwa matibabu kwa gesi huku 30 wakipatiwa matibabu ya kawaida, alipokutana na wahariri wa vyombo vya habari jijini Dar es Salaam.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makala, aliwataka wananchi kuendelea kuchukua tahadhari na kuziagiza taasisi na sehemu zote zenye mikusanyiko kuweko miundombinu nya maji tiririka, kama njia ya kupambana na janga hili.

Waswahili husema tahadhari ni bora kabla ya hatari. Hilo linatishia mwili wa binadamu, kutokana na virusi vinavyoshambulia mfumo wa upumuaji. Swali linabaki, kujiuliza watu waishio maeneo ya mijini, wanapata wapi elimu ya kujikinga na janga hilo?

Mwongozo wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, unalenga kutoa elimu ya kutosha, ikiwamo shule zote za msingi na sekondari, kuwa na namna ya kupambana na ugonjwa huo, ikiwamo kukwepa mikusanyiko isiyo ya lazima.

Hadi sasa serikali inaonyesha misimamo mikali ya kujikinga na virusi hivyo, kwa kuanzia na uongozi wa juu kwa kuonekana kila mara wamevaa barakoa. Hapo inadhihirisha, uongozi ni wito na kioo kwa jamii, kama taswira ya matendo kwa wananchi.

Watanzania wamekuwa na imani ya kumtegemea Mungu katika majanga mbalimbali kama haya, kwa kuambatanisha na jitihada zinazotolewa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, kulikwepa janga hili la virusi vya corona.

Tiba za asili ikiwamo kujifukiza bado ni msaada. Pia, jamii kuendelea kukwepa mikusanyiko, kuvaa barakoa, kunawa maji safi na sabuni kila mara, nayo yaweza ikawa chachu ya kuuondoa kabisa ugonjwa huo kitaifa na hata dunia kwa ujumla.

●**Simu: (255) 714265843**

# Misitu 10 yarasimishwa Lindi kutatua migogoro

**Na Said Hamdani, LINDI**

WIZARA ya Maliasili na Utalii kwa ushirikiano na Shirika lisilo la kiserikali la kushughulikia mnyororo wa thamani kwa mazao ya misitu (FORVAC) la Finland, imerasimisha misitu 10 ya hifadhi wilayani Liwale mkoani Lindi kwa matumizi ya maendeleo.

Lengo lingine ni kuondoa migogoro ya mipaka kati ya wakazi wa sehemu moja na nyingine katika maeneo husika.

Mratibu wa FORVAC, James Mshare, aliyesema hayo jana wakati wa hafla ya kukabidhi vitendea kazi mbalimbali vyenye thamani ya Sh.milioni 100, kwa vikundi 20 vya wajasiriamali wadogo wilayani humo.

Vitendea kazi vilivyokabidhiwa ni kwa ajili ya utengenezaji wa nyungo, vichujia tui linalotokana na zao la nazi, mashine za kuranda mbao, mashine ya kufua umeme, mizinga 40 ya kufuga nyuki, misumeno, vifaa vya kupuliza moshi wakati wa kulina asali, mavazi na kofia.

Vingine ni kofia, viatu (gambuti) kwa ajili ya kujikinga jua, miba na wadudu wakali watambaao chini na pikipiki tatu (guta) zenye matairi matatu.

Alisema miezi minne iliyopita kwenye mchakato wa kuhakikisha misitu iliyopo inatambuliwa kisheria ambayo baadhi ni Kokoriko, Muungurumo, Nambikia, Nandete na Mbila.

Alisema misitu hiyo imerasimishwa kwa namba 454, Juni 25 mwaka huu na kwamba hakuna mtu, kikundi au taasisi itakayobadilisha matumizi ya Ardhi ya Misitu hiyo, bila kupata kibali.

Awali, Mkuu wa Wilaya ya Liwale, Judithi Nguli, alishukuru FORVAC kwa kusimamia mchakato huo na kwamba itasaidia serikali kupunguza gharama za upimaji.

Aidha, aliwataka wananchi kutoharibu misitu na badala yake wawe mabalozi wazuri wa uhifadhi ili kunufaika na uwapo wake ambao ni pamoja na mvua, vivuli na ajira itakayotokana na mazao ya misitu na hewa safi.

# CCM yajinadi kwa utetezi wa maslahi ya umma

**Na Mwandishi Wetu,** RUKWA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimesema hakitaacha kutetea maslahi ya umma, kupigania maendeleo ya kisekta au kutofuatilia ahadi zilizotolewa wakati wa uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.

Hayo yalisemwa jana na Katibu wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa (Itikadi na Uenezi), Shaka Hamdu Shaka, wakati akizungumza na wazee, wenyeviti wa mashina, viongozi na wanachama wa chama hicho, Wilaya ya Sumbawanga Vijijini.

Alisema kazi ya CCM tokea enzi za TANU na ASP ni kushughulika na maisha ya watu, shida, kero zao na kutazama kwa kina mikakati ya kimaendeleo iliyobuniwa kisera katika maeneo husika inafanyiwa utekelezaji.

"CCM kazi yake kubwa ni kutazama iwapo mipango na mikakati ya kisera inabeba uhalisia wa utekelezaji katika kutoa majawabu ya kero za wananchi na kuharakisha maendeleo na pale itakavyokuwa vinginevyo hakitakaa kimya kwa kumwonea mtu aibu," alisema Shaka.

Aidha, alisema lengo la wapinzani ni kutaka kuwaondoa kwenye reli ya utekelezaji wa majukumu yao ya msingi na ya kisera, ambayo hata wao wanajua waliyoahidi.

Shaka alisema katika ushindani wowote kila upande huomba washindani wao wadhoofike ili upande wa pili upate sababu za kuwaeleza wananchi kwamba mliowapa dhamana wameshindwa kutekeleza watataka wao waaminiwe na wananchi kushika madaraka ya utawala, jambo ambalo kwa CCM hawawezi kufanikiwa kutokana na umakini wake.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA WILAYA KINONDONI

SAHURI LA MADAI NA. 26 YA 2021

AUA INDUSTRIA GROUP LTD.................................................... MLETA MADAI
DHIDI YA
EMEC ENGINEERIG LTD ....................................................................MJIBU MADAI

Kwa,
EMEC ENGINEERING LTD

KUITWA SHAURINI

Kwa kuwa mleta madai yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika nakala za madai ambazo zinaweza kupatikana katika mahakama hii, kwa hiyo unahitajiwa kihudhuria mahakama hii binafsi binafsi au wakili binafsi au Wakili au Mwakilishi ambaye anaruhusiwa siku ya **tarehe 15 mwezi 07/2021 saa 2:00 Asubuhi.**

Kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kutaja shauri hilo ni lazima ulete hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.

ANGALIZO:
Kama hukudhuria siku iliyotajwa hapo juu na Mahakama ikithibitisha kama umepokea wito wa kuitwa shaurini itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe **01 mwezi 07 mwaka 2021.**

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA WILAYA
KINONDONI

116348702


# Agizo kituo cha huduma ya pamoja kufanya kazi saa 24

**Na Romana Mallya**



KATIBU Mkuu wa Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Zainabu Chaula (pichani), ameagiza taasisi zinazowahudumia wananchi kupitia kituo cha huduma ya pamoja kilichofunguliwa ofisi za Posta Tanzania kuangalia uwezekano wa kuzitoa saa 24 ili wananchi wasikwamishwe.

Dk. Chaula aliyasema hayo baada ya kutembelea ofisi za Shirika la Posta, Dar es Salaam ambapo huduma hizo zimeanza kutolewa rasmi kuanzia mwanzoni mwa mwezi huu ikiwa ni ahadi ya serikali.

Alisema huduma hizo zimeanza katika ofisi mbili za Posta ambazo ni Dar es Salaam na Dodoma na wamelenga zisambae nchi nzima.

"Hapa kuna TRA (Mamlaka ya Mapato Tanzania), NSSF (Shirika la Hifadhi la Taifa), RITA (Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini), NIDA (Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa, BRELA (Mamlaka ya Usajili wa Biashara na Leseni) na Uhamiaji ambapo mwananchi badala ya kwenda kwenye ofisi hizi anakuja hapa Posta anapata huduma zote kwa wakati mmoja," alisema.

Dk. Chaula aliwataka viongozi wa taasisi hizo kuhakikisha wabadilike kwa kuhakikisha huduma zinatolewa saa 24.

"Unakuta mteja amechelewa kwenye foleni anafika hapa unamwambia muda umeisha lazima tubadilike katika utoaji huduma, suala la usalama na muda wa kuingia kazini kwa awamu ni masuala ya kujadiliwa," alisema.

Alisema serikali inatekeleza mradi wake wa Tanzania ya kidigitali na kupitia Shirika la Posta wameamua kuanzisha vituo hivyo.

Kaimu Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania, Macrice Mbodo, alisema kwa sasa huduma hiyo imeanza kutolewa katika ofisi ya Posta Dar es Salaam na Dodoma na wanatarajia hadi mwezi ujao zitasambaa ofisi 10 na baadaye watakwenda nchi nzima.

Alisema lengo ni kuhakikisha wanapunguza muda mwingi ambao wananchi hutumia kwenye ofisi hizo na kusababisha msongamano.

Mkurugenzi Mkuu wa NIDA, Arnold Kihaule, alisema kituo hicho cha pamoja kitasaidia kuongeza ufanisi katika ufanyaji kazi na wamejipanga kutoa huduma kwa kushirikiana na taasisi nyingine.

Ofisa Mtendaji Mkuu BRELA, Godfrey Nyaisa, alisema kituo hicho cha kidigitali kitasaidia kutatua kero walizokuwa wanazipata wananchi kutoka sehemu moja kwenda nyingine ili kuzipata.

Kaimu Kabidhi Wasii Mkuu na Mtendaji Mkuu wa RITA, Emmy Hudson, alisema ndani ya ofisi hizo za Posta watatoa huduma za usajili wa vizazi na vifo na vyeti vyake.

Kamishna wa Uhamiaji, Gerald Kihinga, alisema wataanza kutoa huduma za hati ndogo za kusafiria na baadaye watachakata maombi ya hati kubwa za kusafiria.


(NBAA)
BODI YA TAIFA YA WAHASIBU NA WAKAGUZI WA HESABU TANZANIA

TANGAZO LA MNADA

Wananchi wote wanatangaziwa kwamba, Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA) itauza kwa njia ya mnada wa hadhara gari moja chakavu aina ya **Toyota Land Cruiser Station Wagon GX-STD katika Mkoa wa Dar es salaam. Mnada utafanyika Mhasibu House, Mtaa wa Bibi Titi Mohamed, Upanga – Dar Es Salaam 23/07/2021 kuanzia saa 4:00 asubuhi.**

**Masharti ya Mnada:**
1. Gari itauzwa kama lilivyo na mahali lilipo
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa papo hapo amana (deposit) isiyopungua asilimia ishirini na tano (25%) ya thamani ya gari, na kukamilisha malipo yote katika muda wa siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya mnada. Mnunuzi akishindwa kutimiza malipo yote katika muda uliopangwa, atakosa haki zote za ununuzi wa gari hilo na amana (deposit) yake haitarudishwa.
3. Mnunuzi atakayeshindwa kulipa amana (deposit) ya asilimia ishirini na tano (25%) papo hapo atachukuliwa kuwa na nia ovu ya kuharibu mnada hivyo hatua kali za kisheria zitachukuliwa juu yake kwa mujibu wa Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
4. Mnunuzi atatakiwa kuondoa gari alilonunua katika muda wa siku saba (7) tangu kukamilisha malipo.
5. Ruhusa ya kukagua gari itatolewa siku mbili kabla ya tarehe ya mnada

MKURUGENZI MTENDAJI,
BODI YA TAIFA YA WAHASIBU NA WAKAGUZI WA HESABU
4 BARABARA YA UKAGUZI, "AUDIT HOUSE", GHOROFA YA NANE,
S.L.P. 1271,
41104 TAMBUKARELI,
DODOMA, TANZANIA
SIMU.: +255 26 2160170 - 4
BARUA PEPE: info@nbaa.go.tz
TOVUTI: www.nbaa.go.tz

216351102

# Waziri aridhishwa utengenezaji matela

**Na Beatrice Shayo**

WAZIRI wa Biashara na Viwanda, Prof. Kitila Mkumbo, amesema kutengenezwa kwa matela ya magari nchini, kutasaidia kutatua tatizo la usafirishaji wa mazao ya wakulima.

Mkumbo aliyasema hayo jana wakati akizindua tela lililotengenezwa nchini katika Maonyesho ya 45 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam (DITF), maarufu kama Sabasaba.

Alilipongeza Shirika la Maendeleo ya Taifa (NDC) kwa kubuni tela hilo na kushirikiana na taasisi mbili kwa ajili ya kutengenezwa nchini.

"Hii inaonyesha viwanda vyetu vinaweza kutengeneza bidhaa za msingi na moja ya malengo yetu ni kukidhi mahitaji soko la ndani ili tuanze kutumia na kula bidhaa ambazo tunatengeneza sisi wenyewe," alisema Mkumbo.

Alisema tela hilo linahitajika kwa wakulima kwa ajili ya kusafirisha mazao yao na kwamba ni jambo jema kutengenezwa nchini na gharama zake za Sh. milioni 8.3 ambazo ni nafuu.

Naye Kaimu Mkurugenzi Mwendeshaji wa NDC, Rhobi Sattima, alisema Kilimanjaro Machine Tools (KMTC) ni moja ya viwanda vinavyosimamiwa na NDC ambacho kiko wilayani Hai mkoani Kilimanjaro, kitasaidia kuongeza thamani ya uzalishaji hasa katika sekta ya kilimo.

Alisema moja ya vikwazo vikubwa ni usafirishaji mazao na bidhaa mbalimbali ambazo zinakuwa zinaharibika au kutokufika katika maeneo husika kwa sababu ya kukosa vifaa vya usafirishaji.

Sattima alisema kiwanda hicho kinajihusisha na uzalishaji wa mashine za aina mbalimbali pamoja na vipuri vya mitambo ya viwanda na usafirishaji.

"Bidhaa hii ya tela ni moja ya bidhaa zinazozalishwa na kiwanda hiki kwa lengo la kuwawezesha wakulima kusafirisha mazao na pembejeo katika sekta ya kilimo," alisema.

Alisema tela hilo lenye uwezo wa kubeba tani tano, limebuniwa kwa kuzingatia vigezo vyote vya ubora, ufanisi na usalama wakati linapokuwa linafanya kazi na kuthibitishwa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS).

Tela hilo, alisema mchango wake katika uchumi ni kupunguza gharama za kusafirisha mazao na mizigo kwa wakulima, kuongeza kipato na mkulima kulitumia kwa shughuli zingine za uzalishaji kwa kipindi cha mwaka mzima.

"Haya ni mapinduzi kwenye sekta ya kilimo kwani mkulima anaweza kuzalisha bila kuwa na changamoto ya usafirishaji wa mazao na pembejeo.

Hii itasaidia kupatikana kwa urahisi malighafi za kilimo kwa ajili ya kuongeza thamani katika viwanda," alisema.




Wananchi wakipata maelezo kuhusu shughuli za kampuni ya Barrick, walipotembelea Maonyesho ya 45 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam yanayoendelea katika Viwanja vya Mwalimu Nyerere Barabara ya Kilwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watumishi Wanging'ombe watakiwa kuongeza kasi

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WATUMISHI Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe mkoani Njombe, wametakiwa kuongeza kasi ya kuhudumia wananchi baada ya kupata jengo la kisasa.

Agizo hilo limetolewa jana na Katibu Tawala wa wilaya hiyo, Edward Manga, kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya, Lauteri Kanoni wakati wa makabidhiano ya jengo jipya la ofisi lililogharimu zaidi ya Sh. bilioni mbili, lililojengwa na Shirika la Nyumba (NHC).

Alisema serikali wilayani humo inaamini kuwa kukamilika kwa jengo hilo kutaongeza ufanisi.

Manga alisema ujenzi wa jengo hilo ni mojawapo ya mradi mkubwa uliyogharimu kiasi kikubwa cha fedha na kuongeza hadhi ya halmashauri ya wilaya hiyo.

Alisema, jengo hilo limejengwa kwa viwango stahiki kwa kuwa mpaka kukamilika kwake limekuwa likisimamiwa na wakala wa majengo Tanzania (TBA).

Aliwataka watumishi watakaotumia jengo hilo kujenga nidhamu na kulitunza ili liendelee kuwa kivutio kwa watumishi na wananchi wanaopatiwa huduma.

Pia alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kuridhia kutengwa fedha ili kuleta mradi huo mkubwa wa mabilioni kwenye wilaya hiyo ya Wanging'ombe.

Mwakilishi wa NHC, Mhandisi Abdul Kambwele, alisema mradi huo ulianza mwezi Agosti mwaka 2018 na kukamilika mwezi Novemba 2020.Alisema mradi huo umegharimu Sh. 2,748,230,000 na hadi kukamilika kwa jengo hilo NHC imepokea Sh. 2,523,403,649 kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe sawa na asilimia 92 ya mkataba.

"Tulihakikisha tunapata kibali cha kuendelea na ujenzi baada ya ukaguzi kutoka kwa mshauri elekezi ambaye ni TBA," alisema Kambwele.

Ofisa Mipango wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Emmanuel Kilundo, alisema wakati halmashauri hiyo inaanzishwa mwaka 2013 haikuwa na majengo yake na kulazimika kutumia yaliyopo chini ya Kanisa Katoliki Njombe.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe Agnetha Mpangile, alisema wilaya hiyo ni mpya inahitaji majengo mengine ili kusogeza huduma karibu na wananchi ambazo nyingine bado wanazifuata mbali.

# Wapewa ofa vivutio utalii

**Na Elizabeth Zaya**

WAKALA wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), imetoa ofa maalum kwa watu wanaotembelea banda lao katika Maonyesho ya 45 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam kwenda kutembelea vivutio vya utalii Julai 10 na 17 mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Meneja Uhusiano wa TFS, Martha Chasama, alisema wametoa ofa hiyo kwa watakaotembelea banda lao na kujisajili kwa ajili ya kwenda kutembelea vivutio hivyo.

"Tumeona tutumie fursa hii kuwapeleka watalii wanaopenda kwenda kutembelea vivutio vyetu wawe ni wa kutoka ndani ya nchi au nje ilimradi tu waje kujisajili katika banda letu, na gharama tumeweka kidogo sana tofauti na ambavyo huwa tunafanya, hii ni ofa ya Sabasaba tu," lisema Chasama.

Alitaja maeneo ya vivutio vya kutembelea ambavyo wamevitoa katika kipindi hiki cha Sabasaba ni Kaole, Mji Mkongwe Bagamoyo na Pugu Kazimzumbwi.

Pia alisema TFS imeandaa tukio la kuhamasisha watu kutembelea vivutio vya utalii na namna ya kuhifadhi ikolojia inalojulikana kama West Kilimanjaro Run and Mountain Forest Bike, linalotarajiwa kufanyika Julai 10, mwaka huu.

Chasama alisema lengo ni kutaka watu wajifunze maliasili ambazo Tanzania imejaliwa na namna ya kuzitunza kwa ajili ya vizazi.

Ofisa Utalii wa shamba la Miti la West Kilimanjaro, Mensieur Elly, alisema watakaoshiriki katika tukio hilo watatembelea maeneo mbalimbali ya vivutio ikiwamo mapango, mabwawa na katika maeneo ya maporomoko.

"Pia katika tukio hili tunatarajia kuwa na mbio za kilomita tano, 10 na 22 za wakimbiaji, na kwa waendesha baiskeli wataendesha kilomita 10 na 22 na watu wengine ambao hawatakimbia wala kuendesha watatembea kilomita tano," alisema

HABARI KITAIFA

# TADB kuwapa mikopo wakulima wa zabibu

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

BENKI ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), imewahakikishi wakulima wa zao la zabibu kupata mikopo itakayosaidia kuongeza uzalishaji na mnyororo wa thamani ya zao hilo ambalo ni miongoni mwa mazao ya kimkakati hapa nchini.

Akizungumza baada ya mkutano na wadau wa zao hilo ulioitishwa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa juzi jijini hapa, Mkurugenzi Mtendaji wa TADB, Japhet Justine, alisema benki yake itaendelea kutekeleza mikakati ya serikali ya kukuza sekta ya kilimo kwa kutoa mikopo, ambayo itasaidia kuongeza uzalishaji na kuwaunganisha wakulima wengi kwenye mnyororo wa thamani wa mazao.

"Miongoni mwa malengo ya kuanzishwa kwa benki hii ni pamoja na kuhakikisha inachangia kwa kiasi kikubwa katika kuleta mapinduzi yenye tija katika sekta ya kilimo nchini kwa kuwezesha upatikanaji wa mikopo. Tunawahakikishia wakulima wa zabibu mikopo yenye masharti nafuu na ambayo itasaidia kuongeza uzalishaji wa zao hilo muhimu," alisema Justine.

Aliwataka wakulima kuondoa hofu ya kukosa mikopo kwa kigezo cha kukosa dhamana kwani kinachomfanya mkulima akopeshwe na benki hiyo ni uwezo wa mradi husika.

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI), Dk. Geofrey Mkamilo, alisema kuna upungufu katika uzalishaji wa miche ya zabibu na kwamba wataendelea kufanya utafiti wa mbegu bora zaidi na kuzizalisha kwa wingi zaidi ili kukidhi mahitaji ya ndani.

# Vijana Msalala wapata mkopo wa pikipiki 20

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

HALMASHAURI ya Msalala wilayani Kahama mkoani Shinyanga, imetoa mkopo wa pikipiki 20 kwa kikundi cha vijana 10 Kata ya Bulyanhulu wanaojihusisha na biashara ya usafirishaji wa abiria, wenye thamani ya Sh. milioni 50, fedha kutoka asilimia kumi ya mapato ya ndani ya halmashauri hiyo.

Pia halmashauri hiyo imebadili mfumo wa utoaji wa mikopo kwa kundi la vijana kwa kuwapatia vitendea kazi badala ya fedha taslimu kama ilivyokuwa awali, baada ya kubaini wengi wao kutumia mikopo wanayopatiwa kinyume cha maelekezo ya katiba ya vikundi vyao.

Akikabidhi pikipiki hizo jana Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo, Simon Berege, mbele ya Mkuu wa Wilaya ya Kahama Festo Kiswaga, alisema katika kikundi hicho cha vijana 10 kila mmoja anapata pikipiki mbili, hatua ambayo itasaidia kurejesha mkopo huo kwa haraka zaidi.

Alisema, vikundi vya vijana vimekuwa vikishindwa kupata mikopo kutokana na wengi wao kutokuwa waaminifu wanapopatiwa mikopo wamekuwa wakigawana na kushindwa kuanzisha biashara na kuisababishia serikali hasara, kutokana na kushindwa kulipa madeni yao.

Kiongozi wa waendesha bodaboda, Bulyanhulu Zephania Bundala, alisema, awali walikuwa wanakopeshwa pikipiki kwa riba kubwa kutoka kwa watu binafsi.



Katibu wa Chama cha Wafanyakazi wa Viwanda, Biashara, Taasisi za Fedha, Huduma na Ushauri (TUICO), Mkoa wa Kinondoni, Caroline Mutembei (kulia), akikabidhi cheti cha mfanyakazi bora kwa Saleh Minangu wa Kiwanda cha kutengeneza mabomba cha Tanzania Steel Pipe (TSP), katika hafla iliyofanyika kiwandani hapo Ubungo, Dar es Salaam juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Lubinga akemea wapika majungu

**Na Jacqueline Liana,** SUMBAWANGA

KATIBU wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM, Kanali mstaafu Ngemela Lubinga, amewataka viongozi na watendaji wa chama hicho kuepuka majungu.

Lubinga alisema hayo juzi alipokuwa akizungumza na wanachama wa CCM katika ngazi za mashina wilayani Sumbawanga Mjini, mkoani wa Rukwa.

Alisema CCM ina utaratibu mzuri wa kushughulikia changamoto za viongozi na watendaji wake, hakuna haja ya kupigana majungu.

Kiongozi huyo aliwataka wana-CCM kuonyeshana upendo na iwapo atatokea mwenye kwenda kinyume na maadili ya chama, arekebishwe kwa staha kupitia vikao vya chama.

Kuhusu masuala yanayozungumzwa na kujadiliwa katika vikao hivyo, alisema wajumbe wanapaswa kuwa na vifua vya kutunza siri kwa kuwa ni kinyume cha maadili kutoa siri za vikao.

Alisema moja ya sifa ya kiongozi bora ni uwezo wa kutunza siri kwa masilahi ya CCM.

Kuhusu uchaguzi wa viongozi wa CCM katika ngazi mbalimbali utakaofanyika mwakani, Kanali mstaafu Lubinga, aliwataka wanachama wa CCM kuwachagua wagombea watakaokuwa watumishi wazuri wa CCM.

Alisema wapo viongozi na watendaji wa chama 'huwabeba' wagombea na kusababisha mitafaruku isiyo na tija kwa chama.

Kiongozi huyo alifafanua kwamba, tabia hiyo ni miongoni mwa sababu za uwepo wa makundi yasiyo na masilahi kwa chama na wanachama, hapana budi ikome.

"Viongozi tusibebe wagombea, ukibeba mgombea umepoteza sifa ya kuwa kiongozi na mtendaji wa chama chetu," alionya.

Kuhusu changamoto zinazowakabili wanachama na wananchi kwa jumla, aliwataka viongozi na watendaji wa CCM kutenga muda wa kusikiliza kero na kuzitafutia majawabu.

Alisema, ilani ya uchaguzi ya CCM ya 2020-2025, imelenga kuondoa kero mbalimbali katika jamii, hivyo utekelezaji wake unapaswa kusimamiwa kwa makini.

Alisema ilani hiyo ina ahadi za maendeleo zinazotekelezwa nchini kote, ni wajibu wa viongozi na watendaji wa CCM, kuanzia ngazi za mashina, kuhakikisha zinatekelezwa kwa ufanisi.

Alifafanua kwamba serikali inatoa fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo, hivyo ni lazima zitumike kwa kusudi hilo.

Pamoja na kuzungumza na wanachama wa CCM katika ngazi za mashina, pia kiongozi huyo alikagua na kushiriki katika ujenzi wa madarasa shule za msingi za Isale na Manga za Sumbawanga Mjini.

# Waziri aridhishwa usalama, afya viwanda vya chuma

**Na Frank Monyo**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu, Kazi, Vijana na Wenye Ulemavu), Jenista Mhagama, ameeleza kuridhishwa na maboresho ya miundombinu ya usalama na afya katika viwanda vya chuma mkoani Pwani.

Alitoa kauli hiyo baada ya kuhitimisha ziara yake katika viwanda vya nondo vya Fujian Hexiangwang na Lodhia Group of Companies vilivyopo Wilaya ya Mkuranga ambapo pamoja na hatua iliyofikiwa, alivitaka kufanya maboresho zaidi.

"Nimefarijika sana kuona yale maboresho ambayo wataalamu wetu wa OSHA waliyatoa ili kuboresha hali ya afya na usalama kwa wafanyakazi yametekelezwa kwa zaidi ya asilimia 70," alisema.

Hata hivyo, alisema bado kuna mambo ambayo waendelee kuyaboresha ikiwamo kuweka mtambo wa kukusanya moshi ili usiharibu mazingira pamoja na afya za wafanyakazi.

"Kitu kikubwa kilichonifurahisha katika kiwanda hiki cha Lodhia Group of Companies ni jinsi teknolojia wanayotumia katika uzalishaji inavyosaidia katika kukuza uchumi wa nchi; kiwanda hiki sasa kinazalisha nondo adimu zenye ukubwa wa milimita 40 ambazo zinauzwa hata nje ya nchi yetu," alisema.

Katika ziara hiyo waziri aliambatana na Kaimu Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA), Khadija Mwenda, ambaye alisema ziara hiyo ililenga kufuatilia utekelezaji wa maagizo mbalimbali ambayo taasisi yake imekuwa ikiyatoa katika viwanda hivyo.

## DIT yaonya kasumba ya bidhaa kutoka nje

**Na Elizabeth Zaya**

TAASISI ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT), imewataka Watanzania kuamini bidhaa zinazotengenezwa na kuzalishwa na wataalamu kutoka ndani ya nchi, kwa kuwa hazina utofauti na zile zinazozalishwa nje.

Ushauri huo ulitolewa na Mkuu wa taasisi hiyo, Prof. Preksedia Ndomba, ndani ya banda lao kwenye Maonyesho ya 45 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam (DITF).

Prof. Ndomba alisema bidhaa zinazozalishwa DIT ni kama zile zinazotoka nje ya nchi na kwamba pamoja na ubora wake, bado kuna kasumba ambayo haijafutika miongoni mwa Watanzania kuamini bidhaa za nje kuliko za ndani.

Alisema asilimia kubwa ya bidhaa zinazohitajika kwa Watanzania zinatengenezwa na wataalamu kutoka ndani ya nchi wakiwamo wanaonolewa na DIT, na kwamba hakuna haja ya wananchi kuendelea kupoteza gharama zao kuagiza bidhaa nje ya nchi.

Mkuu wa Kitengo cha Mahusiano na Viwanda wa DIT, Dk. John Msumba, alisema wamekuwa wakijitahidi kuhakikisha kila maonyesho wanaenda na bishaa mpya na kwa mwaka huu wamepeleka nyingine muhimu ikiwamo mashine ya kuchakata plastiki na kutengeneza vipuli.

## TALIRI kuwainua wafugaji kiuchumi

**Na Elizabeth Zaya**

TAASISI ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI) imesema imepania kuinua hali ya uchumi ya wafugaji kwa kuwapa mbinu bora za ufugaji.

Akizungumza jana katika Maonyesho ya 45 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam (DITF), Mtafiti Mwandamizi wa Mifugo kutoka taasisi hiyo, Valentino Urasa, alisema ina vituo saba ambavyo pamoja na shughuli yao kuu, imekuwa ikiwaelimisha wafugaji kufuga kwa tija.

Urasa alisema lengo la taasisi yao ni kuona wafugaji wanafuga mifugo iliyo bora na yenye kuleta tija ya kukuza uchumi wao na wa nchi kwa ujumla.

"Taasisi yetu inatoa huduma ya ufugaji katika kanda zao mbalimbali na kila mara tunapita kwa wafugaji kutoa elimu kwa sababu tunataka waachane kabisa na kufuga kizamani bila faida," alisema Urasa.

Mtafiti wa taasisi hiyo, Walter Mangesho, aliwahamasisha wafugaji kuhakikisha wanatumia teknolojia ya matumizi ya malisho bora ili kuhakikisha mifugo inakuwa na afya bora na kuwaletea faida kubwa.

Alisema teknolojia hiyo ya malisho bora kwa mifugo ni kuhakikisha wanaotesha majani ya kisasa yenye virutubisho kwa ajili ya mifugo hiyo.




Wananchi wakiangalia bidhaa kwenye banda la wafanyabiashara kutoka China, katika Maonyesho ya 45 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam, yanayoendelea kwenye Viwanja vya Mwalimu Nyerere, Barabara ya Kilwa jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Wanafunzi wabunifu MNMA wavutia Sabasaba

**Na Romana Mallya**

WANAFUNZI wa Stashahada kutoka Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (MNMA) wamevutia mamia ya watu katika viwanja vya Sabasaba baada ya kubuni ubao shuleni unaojifuta wenyewe, kifaa cha umwagiliaji kinachojiendesha na fimbo kwa wenye uoni hafifu.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti viwanjani hapo, katika Maonyesho ya 45 ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam yanayoendelea, wanafunzi hao walisema ubunifu huo umechukua kati ya miezi mitatu hadi mwaka na gharama za kutengeneza hazifiki Sh. 400,000.

Ashiraf Seleman, anayechukua Stashahada ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), alisema amebuni fimbo maalum kwa wenye uoni hafifu ambayo inamwongoza mtumiaji na endapo atakutana na kizuizi wakati akitembea itatetema au alamu.

"Endapo akiwa katika matembezi yake akapotea kuna kifaa nimekifunga eneo analoshikia ambapo atabonyeza kitufe kisha ujumbe mfupi utawafikia ndugu zake zaidi ya mmoja kwenye simu zao na kama ana simu janja 'smart phone' wakati anatuma ujumbe kuna kiunganishi kitakachoonyesha eneo alipo," alisema. Seleman alisema ametumia miezi miwili hadi kuikamilisha fimbo hiyo na kwamba kwa sasa uwezo alionao ni kuzitengeneza 20 kwa mwezi, lengo kuliwezesha kundi hilo kutembea kwa amani kama watu wengine wawapo katika mihangaiko yao ya siku. Johas Katial, anayesomea TEHAMA, alisema amebuni mfumo wa kumwagilia mashamba bila mhusika kuwapo shambani.

"Mfumo huu unajiendesha wenyewe mmiliki wa shamba akiwa anaendelea na majukumu mengine ofisi au nyumbani, akifunga kifaa hiki katika shamba lake udongo unapokuwa mkavu kinawaka chenyewe na kitatuma ujumbe kwa mmiliki," alisema.

" 'Shamba linamwagiliwa' na baada ya udongo kupata maji yanayotosha kitatuma ujumbe kwa mmiliki, 'shamba limeshamwagiliwa' na kitajifunga chenyewe."

Alisema aliamua kubuni kifaa hicho kilichotumia gharama ya Sh. 300,000 kwa sababu wamiliki wengi wa mashamba wakati mwingine hukuta mazao yao yanakauka kutokana na kukosa maji kwa kushindwa kumwagilia kwa wakati.

Mratibu wa Mafunzo ya Shahada za Awali MNMA ambaye ni mwenyekiti wa kamati wa chuo hicho katika maonyesho ya Sabasaba, Dk. Samweli Lunyelele, alisema miradi hiyo imelenga kutatua matatizo mbalimbali yanayoikabili jamii.

Alisema chuo hicho pamoja na mafunzo mbalimbali wanayotoa, wanawezesha wanafunzi kubuni teknolojia mbalimbali ambazo zinaleta hamasa kwa jamii.

## Umati ulivyofurika maonyesho ya Sabasaba

**Na Elizabeth Zaya**

UMATI ulifurika juzi katika Maonyesho ya 45 ya Biashara ya Kimataifa Dar es Salaam (DITF), katika viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere.

Juzi ndio ilikuwa siku maalum ya Sabasaba na Nipashe ilishuhudia idadi kubwa ya watu ikimiminika katika mabanda mbalimbali.

Miongoni mwa mabanda yaliyoonekana kuwa na mwitikio mkubwa ni ya Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) na Wakala wa Usajili wa Vizazi na Vifo (RITA).

Mabanda mengine ni la Maliasili na Utalii ambako idadi kubwa ya watu ilikuwa ikimiminika kwenda kuangalia vivutio vya utalii, Wizara ya Ardhi watu wakimiminika kuomba hati, banda la wasanii, kampuni za simu, mabanda ya wajasiriamali wa viungo na nguo.

Kwa mujibu wa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE), maonyesho hayo yanatarajiwa kufungwa rasmi Julai 13.

Nchi saba na kampuni 76 kutoka nje ya Tanzania zinashiriki katika maonyesho hayo.

Pia washiriki wa ndani katika maonyesho hayo kwa mwaka huu ni 3,002 ikiwa ni pamoja na kampuni za ndani, wafanyabiashara wa kati, wajasiriamali, taasisi za umma na binafsi huku kaulimbiu ya maonyesho hayo ni 'Uchumi wa Viwanda kwa ajira na biashara endelevu,' ikilenga kutambua mchango wa sekta ya viwanda katika kuongeza ajira na uzalishaji wa mazao ya kilimo, madini, uvuvi, mifugo, misitu na kuchochea biashara kwa maendeleo ya uchumi.

Maonyesho yana mitaa maalum ambayo imeandaliwa ili kutoa fursa kwa wadau wote muhimu katika mnyororo wa thamani wa biashara kutangaza na kunadi bidhaa na huduma zao ili kutoa hamasa ya kibiashara na uwekezaji.

Pia matukio mengine yanayofanyika katika maonyesho hayo ni pamoja na mikutano ya biashara (B2B) kwa njia ya mtandao.



Mapinduzi ya UTT, uwekezaji 'kidogo' kwa vijana na wazee, sasa chanzo kipato cha mwezi Ukurasa 12



Ukurasa 14

## PSSSF yabuni mradi mikopo nafuu ya nyumba na viwanja

BUFE
Ijumaa JULAI 9, 2021
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

UCHUMI

# Vikundi 40 vya Mkuranga vyaneemeshwa mil. 377/- mkopo kisheria halmashauri

- Awamu ya tatu kwa vijana, wenye ulemavu, kinamama

**Na Yasmine Protace, Mkuranga**

MIKOPO ni kitu kinachomsaidia mtu aweze kufanya mabadiliko, ikiwamo katika elimu na makazi. Kumekuwapo aina mbalimbali za mikopo, ambayo inatolewa na kumfanya mtu anufaike maradufu.

Inapotolewa mikopo kwa ajili ya wanafunzi, hiyo inawasaidia wanaolenga jambo fulani, kuyafikia malengo yao.

Msingi una sura kwamba, iwapo mtu anakosa mkopo na akashindwa kuendelea na masomo yake, basi itamfanya mwanafunzi ashindwe kufikia malengo.

Daima, mikopo ya kilimo, nyumba na fedha katika makundi mbalimbali yote ya jamii inapotolewa inakuwa mkombozi kwa wanufaika husika.

Hiyo ni katika sekta kama kilimo, huwa inawasaidia wakulima kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine kirahisi na pasipo vikwazo, wakitimiza azma za kijamii na kiuchumi, vivyo hivyo, mikopo hiyo inapotolewa husaidia makundi mengi kujikwamua kiuchumi.

Katika kuhakikisha makundi ya vijana, wanawake, kumekuwapo na taasisi mbalimbali za fedha ambazo zinayasaidia makundi hayo yaweze kunufaika na mikopo tajwa.

Mbali na taasisi hizo, pia hata serikali kupitia halmashauri zake, imekuwa ikitenga asilimia ya fedha za makusanyo yake kwa ajili ya kunufaisha makundi hayo yapate mikopo.

Elimu mbalimbali za mikopo imekuwa ikitolewa ili iweze kunufaika.

Hadi sasa, katika baadhi ya maeneo yao, kumekuwapo halmashauri mbalimbali zimekuwa zikiyasaidia, waweze kunufaika nayo.



Kinamama wajasiriamali wa Mkuranga wakiwa katika nyendo za shughuli zao. **PICHA: MTANDAO**

**KUTOKA MKURANGA**

Hivi karibuni Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga, mkoani Pwani, iliitoa mkopo ya shilingi milioni 377 katika makundi ya wajasiriamali.

Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo, Mshamu Munde, anasema wanafanya hivyo kutekeleza sera ya nchi na maagizo ya ilani ya uchaguzi mkuu uliopita, kutoa pesa za mikopo kwa vikundi vya ujasiriamali.

Munde anasema, kupitia mapato ya ndani wameshatoa mikopo isiyo na riba kwa awamu ya tatu mwaka huu.

Mkurugezi Mtendaji huyo aliyewakilishwa na Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii, Peter Nambunga, anasema kuna vikundi 40 vimeshanufaika, vikiwamo vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, huku akitoa tahadhari kuwa pesa hizo sio zawadi kwa walengwa, bali zinapaswa kurejeshwa ili wanufaika wengine wakopeshwe.

Akizungumzia idara yake, Nambunga anasema ni mategemeo yake uongozi wa vijiji na watalaamu watafuatilia kwa karibu maendeleo ya miradi, ili baada ya marejesho wapate mikopo mikubwa na kutunisha miradi.

**KATIBU TAWALA**

Kaimu Katibu Tawala wa Wilaya Johnson Mkuranga, ambaye ni Ofisa Tarafa ya Mkamba aliipongeza halmashauri hiyo kwa kuboresha makusanyo ya ndani hali inayofanikisha mikopo itolewe kwa wakati na kuondoa umaskini.

Ofisa Uchunguzi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkuranga, Hafsa Kitime, anawaonya wanasiasa wasijiingize kuvuruga maendeleo ya vikundi hivyo huku akiweka bayana wakibainika watashtakiwa kwa kosa la matumizi mabaya ya mamlaka.

Pia Kitime anawataka wajasiriamali watakaotumia kinyume mikopo hiyo watakumbana na kosa la uchepushaji fedha.

# MAPINDUZI YA UTT AMIS, UWEKEZAJI 'KIDOGO KIDOGO' VIJANA NA WAZEE, SASA CHANZO KIPATO CHA MWEZI

- Mzee aliyeporomoka, asimulia anavyoinuliwa
- Mstaafu afunguka yake 'anavyokula maisha'

**Na Frank Monyo**

HIVI sasa kuna kundi kubwa la watu waliojiingiza kwenye biashara au ujasiriamali, wakilenga kujikimu kimaisha na kuongeza kipato.

Ni bahati mbaya, wapo wanaoanguka kwa kukosa elimu ya fedha au namna ya kukabili hasara katika uwekezaji.

Kutokana na hilo, kampuni ya UTT AMIS, inatoa elimu ya fedha kwa makundi tofauti na jinsi ya kuwekeza katika mifuko yao, kwa malengo ya baadaye. Pia, kunatolewa elimu ya kukabiliana na athari za baadaye kwenye biashara na maisha.

Mpaka sasa, UTT AMIS iliyo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango, hadi sasa ina jumla ya mifuko sita ambayo ni: Umoja, Watoto, Wekeza Maisha, Kujikimu, Ukwasi na Hati Fungani.

Mzee Waziri Kahela (70), mkazi wa Mabibo Dar es Salaam anasema amenufaika na elimu ya uwekezaji kutoka UTT AMIS, akikumbuka.

Anakumbuka alivyofanya biashara kwa mazoea bila malengo ya muda mrefu, pia faida aliyopata alitumia kihiolela, yote yakiishia kuyumba kibiashara, hasa kipindi alichokiita 'cha majanga.'

Mzee Kahela anakumbuka alivyofuga kuku wa mayai na nyama na msimu wa mvua alipata hasara kubwa itokanayo na mafuriko.

Anaeleza: "Nilikuwa na kuku zaidi ya 10,000 ambao walifikisha muda wa kuuzwa."

Anaendelea: "Ghafla mvua ikaja na kuwasomba wote na kila kitu kwenye banda na kuharibu ndoto zangu, nikarudi nyuma sana katika biashara yangu, kwani sikuwa na utaratibu wa kuweka akiba kutokana na faida ninayopata."

Mjasiriamali huyo anasema ndio ulikuwa mwanzo wake kusaka elimu kutoka UTT AMIS, kuhusu kugawanya faida ya biashara, ikiwa namna ya kukabili majanga yanapotokea.

Mzee Kahela, anakumbuka faida zake baada ya elimu kutoka UTT AMIS, kugawanya mtaji kwenye mifuko mitatu ya UTT: Maisha, Jikimu na Watoto, akinuia kujihami na majanga, hali kadhalika biashara ya sasa na baadaye.



Ofisa kutoka kampuni ya UTT AMIS, akitoa elimu kwa watoto kuhusu umuhimu wa kuweka akiba na kufunguliwa akaunti. **PICHA ZOTE: FRANK MONYO**

> **"Changamoto hiyo ilikuwa... kwamba je, baada ya hatua hiyo na kufunguka kwa uchumi wa soko, huyu mwananchi wa Tanzania anapata manufaa gani na uwepo wa masoko ya fedha na mitaji?**



Ofisa Mwandamizi wa Masoko na Uhusiano wa UTT AMIS, Rahim Mwanga, akitoa elimu ya fedha na uwekezaji katika mifuko ya kampuni hiyo.

### MFUKO WEKEZA

Ofisa Mwandamizi wa Masoko na Uhusiano wa UTT AMIS, Rahim Mwanga, anasema Mfuko Wekeza Maisha una miaka 10 sasa, ukiambatanishwa na faida za bima.

Anasema, mwekezaji katika mfuko huo anaweka lengo la kiasi anachotaka kuwekeza katika muda huo wa miaka 10, kiwango cha chini ni Sh. milioni moja. Ni hiari yake kuwekeza kwa mkupuo au kwa awamu.

"Kwa mfano, mtu ukichagua kuwekeza kiasi hicho (Sh. milioni moja) kila mwezi atahitajika kuwekeza kiasi cha Sh. 8,340 tu ili kukamilisha mpango wake wa uwekezaji.

"Zaidi ya asilimia 99 ya fedha za mwekezaji huwekezwa na chini ya asilimia moja hutumika kugharimia bima," anasimulia akitaja aina ya bima hizo ni za maisha, ulemavu wa kudumu na ajali.

Mwanga anasema baada ya miaka 10 alifungua kiwanda kidogo cha kutotoa mayai ya kuku na kuuza vifaranga pamoja na mayai, akifafanua: "Niliweza kununua mashine (incubator) kwa sasa kipato changu kimeongezeka sana."

### MFUKO JIKIMU

Mwekezaji Kahela anasema, lengo la mfuko ni kukuza na kutoa gawio kutokana na mapato ya ziada kwa vipindi tofauti, pia kumkuzia mwekezaji mtaji.

Anasema, mfuko unatoa fursa mbili za uwekezaji, mapato ya robo mwaka na ya mwaka mzima, kwa kuambatanisha na ukuaji vipande.

Kiwango cha chini cha uwekezaji katika mfuko huo kwa Mpango wa Mapato ya Robo Mwaka, ni shilingi milioni mbili; milioni moja kwa Mpango wa Gawio kwa Mwaka; pia Sh. 5,000 kwa Mpango wa Ukuaji wa mtaji kwa mwaka.

"Kiwango cha chini cha uwekezaji wa nyongeza au unaofuata (additional investment) ni Sh.15,000 kwa mpango wowote wa gawio na Sh.5,000 kwa mpango wa ukuaji mtaji kwa mwaka, hakuna ukomo wa kiwango cha kuwekeza," anafafanua.

### MFUKO WA WATOTO

"Nilijiunga na Mfuko wa Watoto kwa ajili ya ada ya watoto wangu na mahitaji ya shule, kila mmoja nilimfungulia akaunti yake," anasema Kahela na kuendelea:

"Hii ilinisaidia sana, kwani sikupata shida wakati mtoto wangu ameingia sekondari, nilikuwa na uhakika wa elimu bora kwa mtoto wangu kwa sasa wala sina wasiwasi na suala la ada."

Pia, anataja kiwango cha chini cha kuanza kuwekeza ni Sh. 10,000 na kiwango cha chini cha nyongeza ni Sh. 5,000.

Ofisa Masoko Mwanga, anasisitiza kuwa kampuni ya UTT AMIS imechochea maendeleo ya uchumi kijamii na kitaifa kwa ujumla.

Anasema kwa zaidi ya miaka 10 sasa UTT AMIS inasimamiwa na Wizara ya Fedha na Mipango, ikitoa fursa kwa Watanzania wa vipato vyote kuwekeza kwa manufaa yao, watoto, familia na taifa.

### SAFARI INAKOELEKEA?

Mwanga, anasema serikali ililenga wigo mpana kwa umma, kuwawezesha kuweka akiba na uwekezaji kwenye masoko ya fedha na mitaji ili kushiriki kumiliki uchumi nchini na mabadiliko ya sera za kiuchumi katika nyakati hizo.

"Serikali ilitaka kuleta ushiriki mpana wa wananchi, kwenye uchumi kwani kulikuwa na sera ya ubinafsishwaji wa kampuni ya serikali, kukawa na changamoto kubwa kwa Watanzania.

"Changamoto hiyo ilikuwa...kwamba je, baada ya hatua hiyo na kufunguka kwa uchumi wa soko, huyu mwananchi wa Tanzania anapata manufaa gani na uwepo wa masoko ya fedha na mitaji?" Anahoji Mwanga.

### INAFANYAJE KAZI?

Mwanga anasema, UTT AMIS imepewa leseni kutoka Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) kukusanya amana kutoka kwa wawekezaji na kuziwekeza.

"Tukishapata hizo fedha tunaenda kuwekeza katika mfuko husika kulingana na waraka wa toleo la mfuko. Mifuko yetu tuliyonayo inawekeza katika sehemu kubwa mbili ambazo ni masoko ya fedha na masoko ya mitaji.

"Faida inayopatikana inarejeshwa na kugawanywa kwa wawekezaji na sehemu ya uwekezaji wao katika mfuko ndio inafahamika kama kipande," anafafanua Mwanga.

### MASOKO YAKE JE?

Mwanga anaeleza masoko ya mitaji ni fedha inayohusisha dhamana za uwekezaji zaidi ya mwaka mmoja.

"Mfano, kuna kuwekeza kwenye hisa ambazo zimeorodheshwa na Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE), pia kuna kuwekeza kwenye hati fungani za muda mrefu na serikali au zile fungani ambazo mwekezaji anaikopesha serikali kwa muda mrefu na baadaye inamlipa kwa mujibu wa makubaliano," anafafanua.

### FAIDA ILIYOKO

Mwanga anasema faida ya uwekezaji inajumuisha nafasi ya faida ushindani sokoni, pia hatari za uwekezaji zikipunguzwa kwa kufanya uwekezaji mseto

"Mifuko ya uwekezaji inawezesha wawekezaji wadogo kupata fursa za kuwekeza kwenye masoko ya fedha na mitaji kwa viwango vidogo vya fedha tena mara kwa mara.

"Wawekezaji pia wanapata fursa ya kuwekeza kwenye dhamana ambazo katika hali fulani mwekezaji mmoja mmoja inakuwa ni ngumu au ghali kuweza kupata dhamana hizo," anasema.

### WANUFAIKA KIBIASHARA

Mwekezaji Samia Ngonyani, anaeleza: "Nilikuwa na ndoto ya kufanyabiashara ya kuagiza bidhaa kutoka nje ya nchi, lakini baada ya kuibuka kwa janga la corona tatizo la janga la corona, mipaka ikafungwa na biashara zikasimama."

"Kwa hiyo ile pesa niliyotaka kuagizia mzigo ikanibidi niwekeze katika Mfuko wa Ukwasi (liquid fund) huku nikisubiria hali ikae sawa," anaendelea Samia, mkazi wa Mwenge Mlalakuwa, Dar es Salaam.

Anaeleza elimu ya kuweka akiba na kuwekeza alipewa na maofisa wa kampuni hiyo na ndiyo iliyompa mwanga katika safari yake kuwa mfanyabiashara mkubwa, kwani pesa alizowekeza katika UTT inaongeza mtaji wake.

### MNUFAIKA MSTAAFU AFUNGUKA

Fabiani Nyato, ambaye ni mstaafu katika taasisi moja ya kiserikali ambayo hakutaka kuitaja jina lake, amesema kuwa UTT AMIS, anasema imemsaidia kutunza fedha zake za kiinua mgongo kwa faida huku akifanya utafiti afanye biashara gani.

Anasema katika kiinua mgongo alicholipwa, aliamua kuwekeza katika mfuko wa Hatifungani, Ofisa Mwandamizi wa Masoko wa UTT, anasema kuna lengo la kutoa gawio kila mwezi na kila baada ya miezi sita, huku pakiwapo mpango wa kukuza mtaji.

"Nilipostaafu kazi nilifuatilia mafao yangu na nilipata tu. Niliwatafuta UTT AMIS na kuwekeza Sh. milioni 50 ambayo kwa mwezi napokea wastani wa shilingi 500,000 ambayo inanitosha kabisa kufanya shughuli zangu na kuendesha maisha," anasema Mshiyu.

Mwenyekiti wa Kikundi cha Samaria kilichopo Dar es salaam, Nurdin Musini, anasema kikundi chao ni wawekezaji wa UTT AMIS kwa zaidi ya miaka mitatu sasa.


Anasema kikundi hicho kimepata manufaa makubwa kupitia uwekezaji kwani wameweza kufanya miradi mbalimbali ukiwamo wa ufugaji wa samaki.

"Katika kikundi chetu tuna michango ya wiki na ule mkubwa wa mwezi, fedha hizo zote tumekubaliana wanachama wote kutoa asilimia 10 kwa kila michango itakayopatikana na kuwekeza Kampuni ya UTT AMIS kupitia mfuko wa Ukwasi," anasema.

---

## TAFAKURI YA MLALAHOI

# Tunaanza kuwa na nchi ya mabalozi!




**Na Joseph Kulangwa**



**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe: jkulangwa@yahoo.com

MIAKA hiyo tukiwa shule za msingi, tukikimbia mchakamchaka, tulifundishwa kuimba nyimbo za kumshambulia kaburu wa Kusini mwa Afrika, bila hata kumfahamu, tukiimba "Kaburu matata hiya, hiya!"

Kwa kweli sikuwa najua maana yake, ingawa baadaye nikaja kufundishwa mtu anaitwa Ian Smith, eti ndiye alikuwa kiongozi wa makaburu yeye akiongoza Rhodesia Kaskazini, ambayo baadaye tukaja kuambiwa ilibadilishwa na kuwa Zimbabwe.

Lakini, nyimbo nyingi zikielekezwa Afrika Kusini iliyokuwa Rhodesia Kusini, ambako kulikuwapo ubaguzi wa rangi, weusi wakionekana hawana haki tena katika nchi yao, hebu fikiria, mtu anakuja kwenu anakubagueni kwamba hamstahili kupata haki!

Miaka ikaenda huku mjukuu wa Burito na wenzake wakipambana kuikomboa Afrika na hatimaye Afrika ikawa huru, ukabaki ubaguzi wa hapa na pale Afrika Kusini, wakapambana wee mwishowe Madiba akaja akaufutilia mbali na kuleta utaratibu wa maridhiano. Afrika angalau ikatamba kuwa huru.

Katika miaka ya baadaye ya sabini hapa kwetu Bongo, tukiendelea kukimbia mchakamchaka, tukafundishwa nyimbo za 'Amini joka lipigwe'. Ni baada ya majeshi ya Iddi Amini ambaye baadaye tulimpachika jina la Nduli, yalipovamia Kagera na kuwamwaga midomo watani wangu na kuwapora magari (baiskeli) yao.

Amini tukajiaminisha kuwa hana tofauti kabisa na majoka yote unayoyajua duniani, ambayo hayana huruma na binadamu na wanyama wengine.

Alipopigwa na kukimbia, tukashangilia sana, ingawa akatulazimisha kujifunga mikanda kwa miezi 18 ambayo iliamua kudumu hadi leo.

Lakini, ndivyo imani inavyomfanya mtu amwamini mtu au asimwamini. Unaweza kuambiwa ni mbaya ukaamini hata bila kuona ubaya wake na vivyo hivyo ukaambiwa ni mwema bila kuona wema wake.

Ingawa, pia unaweza kuwa shuhuda wa ubaya na wema wa mtu, kama yakikufika. Asifuye mvua huwa imemnyea!

Watanzania hatuchezi mbali na ukweli huo, hasa viongozi wetu ambao wanaweza siku moja wakaamka na kufanya mambo usiamini, kuwa ni wao au wameshauriwa!

Kuna wimbi la uteuzi wa mabalozi siku hizi. Si mabalozi wale anaoteua Mama Samia, la hasha! Mabalozi tu eti wa kutangaza. Wa promo hawa!

Mwaka huu mwanzoni, kuna mheshimiwa waziri aliteua mabalozi wa mazingira, mabalozi wa kusimamia mazingira, majina kibao, wasanii, watu mashuhuri na wengineo, ili mradi majina maarufu yakasheheni. Sina uhakika kama 'wataalamu' hao wa mazingira wameshaanza majukumu.

Ilipoisha hiyo, akaja mwingine kutoka moja ya wilaya za Dar es Salaam, naye akatembelewa na msanii fulani mchekeshaji wa majukwaani kutoka Kenya, akavutiwa na vichekesho, bosi naye akamtangaza kuwa balozi wa wilaya hiyo. Sasa sijui anakwenda kuitanganza vipi Kenya?

Kabla jua halijazama sawasawa, mheshimiwa mwingine naye kaja na mabalozi wake, eti wa kuhamasisha na kuelimisha jinsi ya ulipaji kodi, naye kama mwingine hakusahau wasanii na wachezaji na wachambuzi wa soka! Sijui kama wameshaapishwa ili kuanza kazi.

Ikanikumbusha mheshimiwa aliyeteua wasanii wake akapita akakusanya nguvu za kuwapeka hifadhini na Mlima Kilimanjaro, wengine wakashindwa kupanda, nguvu zingine akapeleka mahali fulani.

Mwenye jukumu lake kusimamia haki ya serikali inaenda sawa, akammulika akasema "sina uhakika na kinachoendelea."

Lakini, jamani ni ugonjwa gani huu sasa umekuja ukiandamana na Uviko-19 ambayo bado inatuhenyesha? Mabalozi hawa wasio hata na utaalamu wa tasnia husika, wanaweza kweli kufanya haya?

Je, wanaowateua wanawajua undani wao au wanaambiwa tu huyu hivi huyu vile? Hatuna wataalamu wa mazingira? Hatuna wataalamu wa kodi? Hatuna wataalamu wa wanyamapori na utalii?

Mbona tuna vyuo vya mazingira, utalii na kodi?

Hivi hakuna vijana waliohitimu walioko mitaani bila kazi, ambao tunaweza kuwageuza mabalozi wakafanya kazi hiyo kitaalamu kuliko wasanii? Kuna vyama vya waandishi wa mazingira, vimetumika? Au mtindo ni kupeana ujiko? Haya bhana twendeni kazi iendelee! Alamsiki!

BIASHARA

# PSSSF yabuni mradi mikopo nafuu ya nyumba na viwanja kibao mikoa 12

## • Yapiga filimbi kuanza, mbia Benki Azania

**Na Christina Mwakangale**

KUMILIKI nyumba ni ndoto ya binadamu wengi, haijalishi kwa walio na kipato cha chini, kati au juu, kwa sababu baada ya pilika za kila siku kutafutia riziki, mwisho wake wanarejea nyumbani.

Hiyo inatokea kwa baadhi kutofikia ndoto hiyo kutokana na sababu tofauti, ikiwamo malengo waliyojiwekea na vipaumbele vyao, ingawa walio wengi tatizo la kiuchumi huwa chanzo.

Gharama za ujenzi na vifaa vinatajwa kuwa ghali, pia ununuzi wa ardhi, ingawa elimu ya namna ya kutoa kipaumbele katika umiliki wa nyumba kutowafikia wengi nayo ni chanzo.

Ndio sababu, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) pamoja na Benki ya Azania, kwa pamoja wamepania kukamilisha ndoto ya Mtanzania kumiliki ardhi kwa kutumia mfumo kila mmoja ataumudu.

Meneja Uhusiano na Elimu kwa Wanachama kutoka Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), James Mlowem, anaiambia Nipashe kwenye Maonyesho 45 ya Biashara ya Kimataifa, Sabasaba, mkoani Dar es Salaam, kwamba mfuko unatoa fursa ya umiliki nyumba za bei nafuu.

Anasema, nyumba yenye thamani ya Sh. milioni 36 hadi Sh. milioni 61 anaweza akamiliki Mtanzania yeyote kwa mkopo kuanza kulipia asilimia 10 pekee ya kiasi hicho na kumaliza deni la nyumba kwa kipindi cha miaka 15.

Mlowe anasema, mradi wa nyumba hizo za gharama nafuu ambazo huduma ya maji, umeme, jirani na barabara zilizo na vyumba viwili hadi vinne zipo mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Shinyanga, Tabora, Mtwara na Iringa.

Anasema mradi mwingine ni wa viwanja vya gharama nafuu vilivyopo katika mikoa ya Ruvuma, Kagera, Tabora, Iringa, Katavi, Morogoro, Dar es Salaam, Rukwa, Lindi na Mtwara.

Mlowe anafahamisha kuwa, ulipaji wa nyumba hizo, ni baada ya mkopaji kulipia asilimia 10 ya gharama ya nyumba na anakabidhiwa funguo. Ulipaji ni katika kipindi cha miaka 15, au pungufu kadri mtu anavyojipanga.

"Kuna dhana iliyozoeleka kwenye jamii kuwa kumiliki au kujenga nyumba ni suala lisilowezekana kutokana na gharama. Mfano, mtu aliyepanga nyumba eneo lolote hapa Dar es Salaam na analipia kila mwezi Sh. 200,000 au 300,000 ndani ya mwaka atakuwa amelipia si chini ya shilingi milioni mbili au tatu.

"Pesa hii kwetu mfuko wetu kwa masharti nafuu, kama nyumba ya Sh. milioni 36, ukilipia asilimia 10 (sawa na shilingi milioni 3.6), unamiliki nyumba na unakabidhiwa funguo uhamie, ingawa hati ya nyumba utapewa ukimaliza kulipia kwa miaka 15," anasema Mlowe.

"Ukipanga unalipa kodi kila mwaka hata upange miaka 10 au 20, lakini ukihama sio yako. Sisi nyumba inaanza kuwa yako,



Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu, Bunge, Kazi, Ajira na Watu wenye Ulemavu), Jenista Mhagama, aliposalimiana na mkazi wa Buyuni, Benjamini Mvungi, alipokagua nyumba za gharama nafuu, katika Mradi wa Buyuni, jijini Dar es Salaam. Picha nyingine, sehemu ya makazi ya mradi huo wa mkopo wa PSSSF. **PICHA ZOTE: MTANDAO**



> **"Kupitia makubaliano, wanachama pamoja na wananchi wengine wasio wanachama watafaidika kwa kukopeshwa nyumba na viwanja kwa riba ndogo ya asilimia 10 kwa mwaka**

ukitoa asilimia 10 pekee ya thamani ya nyumba.

"Nyumba ya shilingi milioni 36, ina vyumba viwili, sebule, choo, stoo na jiko za bei ya shilingi milioni 61 ina vyumba vinne, sebule, choo, stoo, jiko, nyumba hizi zimekamilika mtu anaingia tu."

Anasema, mradi wa viwanja ni kuanzia mita za mraba 800 hadi 2000, pia hukopeshwa kwa mfumo huo kwa kipindi cha miaka miwili, na kwamba ardhi hiyo imepimwa, pia unaruhusiwa kuwekeza.

"Kiwanja cha shilingi milioni nne, ndani ya miezi 24, kiwanja kinakuwa chako. Utakuwa ukiendeleza lakini ni cha kwako tayari. Fursa hii ni kwa Watanzania wote, ili kila Mtanzania awe baba au mama mwenye nyumba," anasema Mlowe.

Anasema umiliki wa nyumba hizo, pia ni fursa kwa watumishi wapya watakwenda mikoa na wilaya tofauti.

### SURA YA MRADI

Mkurugenzi Mkuu wa PSSSF, Hosea Kashimba na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Azania, Charles Itembe, Juni 21 mwaka huu, walitia saini makubaliano ya kuwezesha wanachama na wananchi kukopa.

Ni mkopo kutoka benki katika mfumo wa mikopo ya makazi (mortgage loan), wanunua nyumba na viwanja vinavyomilikiwa na PSSSF, kupitia uwekezaji kwenye sehemu mbalimbali nchini.

Kashimba anasema, miradi hiyo ni ya gharama nafuu katika maeneo tofauti na masharti ya kukopa ni mteja kuweka rehani ya asilimia 10 ya thamani ya mkopo au mali na dhamana kiwango cha juu mteja anaweza kukopeshwa, ni asilimia 90 ya thamani ya nyumba au kiwanja.

"Kupitia makubaliano, wanachama pamoja na wananchi wengine wasio wanachama watafaidika kwa kukopeshwa nyumba na viwanja kwa riba ndogo ya asilimia 10 kwa mwaka," anasema Kashimba.

Anajivuna kuwa ni mchango wa kuweka mazingira wezeshi kwa wananchi wawe na makazi bora yanayotimiza kaulimbiu ya serikali ya "nyumba bora kwa wananchi wote inawezekana."

Mkurugenzi wa PSSSF anaendelea: "Mteja atakapokamilisha malipo yake, atakabidhiwa hati yake ya nyumba au kiwanja na benki ya Azania. Muda wa marejesho ya mkopo ni kipindi kisichozidi miaka 15 kwa mkopo wa nyumba na miaka miwili kwa mkopo wa kiwanja."

Anasema mradi wa nyumba nafuu una nyumba 192 na wa viwanja vipo 886 vilivyo na hati na vitakuwa sokoni vikiuzwa kwa mkopo wa riba nafuu, kwa wanachama na wasio wanachama wa mfuko, kwa kuzingatia vigezo na masharti yaliyowekwa.

### KUTOKA BENKI

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Azania, Charles Itembe, anasema ubunifu wa PSSSF una tija kwa wananchi wote kutokana na masharti yake nafuu.

"Kama mfuko umeonyesha nia njema inayolenga kumuinua mwananchi kwa vitendo na sio kwa maneno, benki pia inaona faraja kuwa sehemu ya mradi, kwani tuna uzoefu wa miaka mingi wa ukopeshaji nyumba Tanzania.

"Benki imeanza kutoa mikopo hiyo tangu mwaka 2005 wakati huo benki nyingine zilikuwa bado hazijaanza kufanya kazi hiyo," anasema Itembe, akifafanua kuwa mkopaji atakuwa na muda wa kutosha kulipa taratibu, ilhali tayari ni mkazi wa nyumba.

"Napenda niwahakikishie Watanzania wanaokuja kuomba mikopo ya nyumba au viwanja, tuko tayari kuwahudumia na mikopo hii inatolewa kwa asilimia 10, hakika ni riba ambayo ni ndogo sana."

"Mkopo huu utakuwa na bima ya mkopo kupitia huduma ya 'bank assurance' inayotolewa na Benki ya Azania, kwa hivyo nyumba yako itakuwa salama kwa majanga mbalimbali yanayoweza kusababishwa na moto au mafuriko," anasema Itembe.



# Waziri ajivunia nyongeza bajeti ya ujenzi barabara

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), amesema anafurahia kuona bajeti ya ujenzi, matengenezo ya barabara na madaraja kupitia Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) imeongezeka kutoka Sh. bilioni 275.03 mwaka 2020/21 hadi Sh. bilioni 752.164 mwaka huu.

Ummy Mwalimu alibainisha hayo jijini hapa juzi alipozungumza na waandishi wa habari.

Alisema miradi itakayotekelezwa katika mwaka wa fedha 2021/22 ni ujenzi wa barabara za lami zenye urefu wa kilomita 250.36 na ujenzi wa barabara kwa kiwango cha changarawe zenye urefu wa kilomita 5,834.95 katika majimbo yote 214.

Pia, alisema kutakuwa na ujenzi wa madaraja makubwa 64 yenye urefu wa zaidi ya mita 20.

Alisema utekelezaji wa kazi hizo utafanyika katika halmashauri na majimbo ya uchaguzi Tanzania Bara na kila jimbo limetengewa wastani wa Sh. bilioni moja.

"Katika nyongeza ya bajeti ya Sh. bilioni 322.158 kutokana na chanzo kipya cha tozo ya simu, kipaumbele ni kuboresha barabara za udongo kuwa za changarawe," alisema.Waziri Ummy alisema TARURA itaajiri wahandisi 200 kwa mikataba kwa ajili ya kuharakisha utekelezaji wa kazi za barabara ili wataalamu wapate uzoefu katika utekelezaji wa majukumu yao.

Vilevile, alisema kuwa baada ya utekelezaji wa bajeti hiyo, mtandao wa barabara za lami utaongezeka kutoka kilomita 2,250.69 hadi kufikia kilomita 2,501.05.

Alisema mtandao wa barabara za changarawe utaongezeka kutoka kilomita 27,809.26 hadi kufikia kilomita 33,644.21 na kutakuwa na ongezeko la madaraja 64 ambayo yatafungua sehemu kubwa ya barabara za vijijini.

Waziri Ummy alisema maelekezo mengine ya serikali kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa ni kuhakikisha malipo ya posho za mwezi kwa madiwani yanafanyika moja kwa moja kwenye akaunti zao kabla au ifikapo tarehe 25 ya kila mwezi.

Hata hivyo, Ummy alisema halmashauri 16 zitaendelea kulipa posho za kila mwezi za madiwani kupitia mapato yao ya ndani.

"Halmashauri hizi ni pamoja na Kinondoni, Temeke, Ilala, Kigamboni, Ubungo, Arusha, Mwanza, Mbeya, Moshi, Kahama, Morogoro, Dodoma, Tanga, Geita, Ilemela na Chalinze," alisema.

Alizitaka halmashauri kuhakikisha malipo ya posho kwa watendaji wa kata ya kila mwezi kiasi cha Sh. 100,000 yanafanyika moja kwa moja kwenye akaunti zao kwa kutumia fedha za mapato ya ndani ya halmashauri ifikapo tarehe 25 ya kila mwezi na si vinginevyo.



Naibu Meya wa Jiji la Dodoma, Emmanuel Chibango, akizungumza na wafanyabiashara wa soko la Sabasaba, wakati akiwahamasisha kulipa kodi ya mabanda yao sokoni hapo jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Mgogoro watatuliwa baada ya miaka 20

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

NAIBU Meya wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Emmanuel Chibago na Ofisa Biashara wa Jiji hilo, Donatila Vedasto, wametatua mgogoro uliodumu kwa zaidi ya miaka 20 kati ya wafanyabiashara wa Soko la Sabasaba na uongozi wa Halmashauri ya Jiji hilo.

Mgogoro huo umepatiwa ufumbuzi baada ya Naibu Meya Chibago na Ofisa Biashara wa Jiji, Donatila, kukaa vikao vya mara kwa mara ambavyo vilikuwa vikilenga kujenga uhusiano mzuri hususan katika ulipaji kodi ya soko hilo.

Katika mkutano wa pamoja uliofanyikia katika ofisi ya soko hilo juzi ukiwashirikisha viongozi wa jiji na wafanyabiashara, Ofisa Biashara Donatila alisema umefika wakati wafanyabiashara wa soko hilo kulipa kodi kwa manufaa ya soko.

"Ndugu zangu wafanyabiashara wa Sabasaba, tumekuwa tukifanya mikutano na vikao mara kwa mara ili kutafuta ufumbuzi wa kulipa kodi ndani ya soko letu.

"Na kulipa kodi ni pamoja na kujisajili ili kila mfanyabiashara aweze kufahamika na aina ya biashara anayoifanya.

"Kwa kufanya hivyo, kutasaidia kuwatambua na wale ambao watakuwa wamejisajili kwa vyovyote vile yanapotokea maboresho, watu hao watapewa kipaumbele tofauti na wale ambao bado hawajajisajili," alifafanua.

Naibu Mstaiki Meya wa Jiji, Chibago, alisisitiza kwa wafanyabiashara hao kuwa ili nchi ipige hatua, ni lazima kodi ilipwe.

"Wafanyabiashara wa Sabasaba tumekuwa tukizungumzia ulipaji wa kodi, ukweli hatuwezi kukwepa ulipaji wa kodi katika eneo hili la biashara, lakini uongozi wa Halmashauri ya Jiji hauwezi kukaa peke yake na kupanga kodi ambayo mnatakiwa kulipa.

"Kinachofanyika ni kushirikishana na kufikia mwafaka kama ilivyofanyika katika mkutano huo," alisema.

# Maelfu wawasilisha malalamiko kwa RC

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

MAELFU ya wananchi wa Mkoa wa Dodoma wameendelea kujitokeza kuwasilisha malalamiko yao kwenye timu ya kusikiliza migogoro ya ardhi iliyoundwa na Mkuu wa Mkoa huo, Anthony Mtaka, huku malalamiko ya madai ya fidia yakiongoza.

Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Dodoma, Thadei Kabonge, akizungumza na Nipashe jana, alisema timu hiyo ilianza kazi Julai 5, mwaka huu.

"Kwa kweli mwitikio ni mkubwa, hatukutegemea kupata idadi kubwa ya wananchi wanaofika kuleta malalamiko ya ardhi.

"Tulijipanga kuwahudumia kwa idadi yoyote bila kujali sikukuu au usiku, na ndio maana tumefanyakazi hata siku ya sikukuu ili kutimiza lengo la kuondoa migogoro ya ardhi," alisema.

Kabonge alisema wananchi wengi wamekuwa wakijitokeza kuwasilisha malalamiko yao kwenye timu hiyo tangu kuanza kazi na wamekuwa wakiwahudumia watu zaidi ya 500 kwa kila siku.

Alibainisha kuwa siku ya kwanza walihudumia wananchi 550 na siku ya pili walihudumia wananchi 506 na idadi hiyo imekuwa ikiongezeka kila siku huku malalamiko ya madai ya fidia yakiongoza.

Alisema timu hiyo inaundwa na wanasheria kutoka Chama cha Wanasheria wa Tanganyika (TLS) ambao wamekuwa wakitoa ushauri wa kisheria na kutoa tafsiri ya kisheria ambayo wananchi hawana uelewa.

Alilitaja kundi lingine kuwa ni mabaraza ya ardhi na nyumba kutoka Kanda ya Dodoma ambayo yanahusika na usuluhishi wa migogoro ya ardhi au mashauri ya kisheria.

Makundi mengine ni kutoka msajili wa hati, wathamini wa mkoa na halmashauri, maofisa ardhi, maofisa mipango miji, wapima ardhi na jopo la wataalamu wa TEHAMA na kwamba kila kundi lina majukumu yake.

Aliongeza kuwa kuna dawati la mapokezi ambalo kazi yake ni kuwasikiliza wananchi wanaofika hapo na kuwaelekeza kwenye idara kati ya hizo zilizotajawa ili kupeleka kero zao na kutatuliwa.

Aliitaja migogoro ya ardhi iliyowasilishwa kwao kuwa mingi ni madai ya wananchi kutoridhika na malipo ya fidia ya ardhi yao iliyochukuliwa na halmashauri husika.

Aliitaja migogoro mingine kuwa ni dhana ya upimaji shirikishi ardhi ya mashamba ya wananchi, wengi wakidai kutoridhika na sehemu ya ardhi iliyochukuliwa baada ya kupimwa.

Mmoja wa wananchi waliojitokeza kuwasilisha malalamiko yao mbele ya kamati hiyo, Abeid Ali, alisema ameridhika na huduma aliyopata na kufurahia utaratibu wa serikali katika kuwahudumia.



# Tulia awezesha ujenzi bweni la wasichana

**Na Grace Mwakalinga,** KYELA

NAIBU Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson kupitia Taasisi yake ya Tulia Trust, ametoa msaada wa Sh. milioni 30 katika Shule ya Sekondari Ipinda Wilaya ya Kyela, kwa lengo la kuanzisha ujenzi wa bweni la watoto wa kike.

Akikabidhi msaada huo jana mbele ya Mbunge wa Kyela, Ally Mlaghila, Dk. Tulia alisema ni kumwezesha mtoto wa kike kusoma kwenye mazingira mazuri, yatakayomsaidia kutimiza ndoto zake za kupata elimu.

Alisema kiasi hicho cha fedha kitasaidia kukamilisha ujenzi wa bweni kwa ajili ya kuwasaidia watoto wa kike kupata muda mzuri wa kujisomea nyakati za usiku na kuondokana na ratiba za kufanya kazi za nyumbani wanaporudi nyumbani.

"Tunapofanya haya ni kutaka kuonyesha kwamba kumsaidia mtoto wa kike kutimiza malengo yake inawezekana kwa sababu tunajua kwamba mabinti wetu hawa wanapitia vikwazo mbalimbali huko mitaani ukilinganisha na mvulana," alisema Dk. Tulia.

Alisema anatamani kuona mabinti wengi wanapata elimu bora na kutimiza malengo waliyojiwekea ili kuwa viongozi wazuri wa baadaye kwa kufuata mfano wa Rais wa Tanzania , Samia Suluhu Hassan ni kiongozi makini anayeliongoza taifa kwa ustadi wa hali ya juu.

"Tulia Trust tunayafanya haya kama sehemu ya kutoa hamasa kwa watu na taasisi nyingine ili kila mmoja kwa nafasi yake kuisaidia jamii ili kupiga hatua kubwa zaidi kwa nchi yetu, ambayo kila mmoja atapata manufaa.

Kwa upande wake Mbunge Mlaghila aliahidi kuhamasisha michango kwa kutafuta wadau ili mabweni yajengwe kwenye shule mbalimbali za sekondari wilayani humo na kuwaokoa watoto na mimba pamoja madhara mengi yatakayokwamisha ndoto zao.




Meneja wa Mauzo kwa Wateja Binafsi wa Benki ya NMB, Janet Nyamko (kushoto), akiwafunda wanachama wa SIDO, kuhusu baadhi ya huduma za kifedha zinatolewa na NMB kwa wafanyabiashara wadogo, kwenye Maonyesho ya 45 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam yanayoendelea katika Viwanja vya Mwalimu Nyerere Barabara ya Kilwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wanaojifungua watoto mgongo wazi wanavyoteseka

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

ASILIMIA 90 ya wanawake waliojifungua watoto wenye tatizo la mgongo wazi wamekimbiwa na wenzi wao, huku sababu ikitajwa ni imani potofu kwamba huenda mwanamke ana mikosi au laana.

Kwa mujibu wa Daktari Idara ya Upasuaji kutoka Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya (MZRH), Dk. Israel Mlabwa, alisema wanawake wengi wanaojifungua watoto wenye tatizo la mgongo wazi hukimbiwa na wenza wao na kuwachia jukumu la kulea familia.

Alisema ni asilimia mbili ya wanaume wanaoendelea kuishi na wake zao bila kujali wamejifungua mtoto mwenye tatizo hilo, huku asilimia nane ya wanaume huamua kuwaolea mwanamke mwingine.

"Tatizo la mgongo wazi kwa watoto bado ni kubwa mkoani Mbeya, nawaomba wazazi unapoona mtoto viungo vyake vya mwili haviko sawa tafadhali mlete hospitali ili apate matibabu, kwani ukimuwahisha anapata matibabu na kupona kabisa," alisema Dk. Mlabwa.

Alifafanua kuwa ni vyema wazazi kwa pamoja kushirikiana ili kumtibu mtoto anayebainika kuwa na tatizo badala ya wanaume kukimbia familia zao wakihofia kupata laana au mikosi, baada ya mtoto mwenye tatizo hilo kuzaliwa.

Aidha, aliwataka kinamama kujenga utamaduni kwa kuhudhuria kliniki wanapokuwa wajawazito ili kupata huduma za kiafya zitakazomlinda yeye na mtoto aliyeko tumboni.

Mratibu wa huduma za chanjo Mkoa wa Mbeya, Dk. Danford Barnabas, aliishauri jamii kuachana na tabia ya kuingiza masuala ya kishirikina kwenye afya za watoto na badala yake wazingatie na kufuata ushauri wa kitaalamu na matibabu ili kuokoa maisha ya watoto wao.

Alisema familia zenye migogoro ndizo zinachangia kuleta madhara makubwa ya kiafya kwa watoto, kwani badala ya kushughulikia au kutibu, wanaanza kulumbana na kushikana uchawi.

"Nina uzoefu na jamii hii ya Mbeya, watu wanaendekeza imani za kishirikina badala ya kuzingatia ushauri wa kitaalamu, vivyo hivyo hata kwenye chanjo tunahamasisha mabinti wa miaka 14 kupata chanjo ya saratani ya mlango wa kizazi, lakini wazazi wao wanawakataza wanadai eti tunawachoma sumu ili kuwaua," alisema Dk. Barnabas.

## Wanawake watakiwa kujitegemea kiuchumi

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WANAWAKE wa Mkoa wa Mbeya wamehamasishwa kumiliki uchumi wao badala ya kutegemea mali kutoka kwa wanaume, ambao baadhi yao huwanyanyasa na kushindwa kutimiza malengo yao ya kujikwamua kiuchumi.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Mbeya ambaye ni Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi, wakati akizungumza na wanawake wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya.

Mhandisi Mahundi alisema nyakati zimebadilika, hivyo ni vyema wanawake wakashikamana na kujenga uchumi wao badala ya kutegemea msaada wa mwanaume.

Katika kuwasaidia na kuwawezesha kiuchumi wanawake wa Mkoa wa Mbeya, Mhandisi Mahundi ameanzisha taasisi yake isiyokuwa ya kiserikali, yenye lengo la kuhudumia wananchi hususani wanawake katika nyanja mbalimbali kama elimu, afya na masuala mengine ya kijamii ilijulikanayo kama Maryprisca Women Empowerment Foundation (MWEF).

Kutokana na kutambua mchango wa wanawake ambao walimwezesha kupata ushindi wa nafasi ya uwakilishi bungeni, alisema alimua kutoa mitungi 104 ya gesi kwa wanawake wa Jiji la Mbeya pamoja na shilingi milioni nane ambapo kila mwanamke atapata shilingi 100,000 ili kufanya shughuli ya kujikwamua kiuchumi.

"Nimekuja kuwashukuru wanawake wa Jiji la Mbeya kwa kunichagua kwa kura nyingi ili niweze kuwawakilisha bungeni... hakika nimewawakilisha vyema nimewaandalia vitu vichache ambavyo ni majiko ya gesi kila mwanamama atapata, shilingi 100,000 kwa kila mmoja wenu pamoja na miche ya parachichi ili mkaendelee kuwa mabalozi wazuri wa utunzaji mazingira, watumiaji wa nishati mbadala pamoja na kuanzisha biashara ndogo za kujiingizia kipato," alisema Mhandisi Mahundi.

Aidha, aliwakabidhi viongozi wa Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT) shilingi milioni nane kwa ajili ya ukarabati wa jengo la ofisi za chama hicho na kuahidi kuwasaidia kupitia taasisi yake. Vilevile, aliahidi kukarabati gari la umoja huo ili lianze kutumika.

Aliwahamasisha wanawake wa UWT kujiunga kwenye vikundi ili kupata fedha kiasi cha shilingi milioni 20 ili kufanya mradi wowote utakaowasaidia kujikwamua na umaskini.

Mwenyekiti wa UWT Jiji la Mbeya, Suma Mwaikambo, alimshukuru Mhandisi Mahundi kwa misaada mbalimbali aliyoitoa na kwamba amekuwa kiongozi wa mfano kwa kuwashukuru wananchi waliompa ridhaa ya nafasi ya ubunge.



# Vitendo vya udhalilishaji vyamsikitisha Mkuu wa Mkoa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

LICHA ya serikali kupambana na vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia bado vitendo hivyo vimeshamiri Zanzibar.

Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Idrisa Kitwana, aliyasema hayo jana huko Maruhubi wakati akitoa taarifa ya utekelezaji wa kazi kwa Julai, mwaka jana hadi Juni mwaka huu wakati Rais wa Zanzibar alipoanza ziara yake katika mkoa huo.

Alisema kwa muda wa mwaka mmoja jumla ya matukio 380 ya udhalilishaji wa kijinsia yameripotiwa katika mkoa huo jambo ambalo ni la kusikitisha.

Alisema katika matukio hayo 241 yanaendelea na upelelezi, 10 yapo kwa mkurugenzi wa mashtaka, 93 yapo mahakamani, 12 yametolewa hukumu, sita yamepatiwa ufumbuzi, saba watuhumiwa wameachiwa huru na 11 majadala yamefungwa.

Akitoa taarifa ya migogoro ya ardhi, Mkuu wa Mkoa huyo alisema malalamiko 188 yameripotiwa katika mkoa huo na 96 yamepatiwa ufumbuzi na 89 yanaendelea kufuatiliwa.

Alisema mkoa huo unakabiliwa na msongamano mkubwa wa watu ambao shughuli zao zaidi ni kilimo, utalii na biashara ili kujipatia kipato.

Aidha, alisema mkoa huo una hoteli 131 za kitalii zenye hadhi tofauti ambazo zimesaidia kutoa ajira kwa vijana.

Alisema kuwa bado mkoa wake unakabiliwa na changamoto ya uhaba wa huduma ya majisafi na salama.



Mwananchi Khamis Ali Haji akitoa malalamiko kuhusu mgogoro wa ardhi mbele ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi (hayupo pichani), alipotembelea vyanzo vya majisafi na salama vya Welezo, akiwa katika ziara ya mkoa wa Mjini Magharibi jana, kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo. **PICHA: IKULU**

# Mwinyi aiagiza ZAWA kutatua tatizo la maji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameitaka Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA), kutatua tatizo la ukosefu wa maji katika maeneo mbalimbali ya mji huo ambayo inakosa huduma hiyo.

Aliyasema hayo jana baada ya kusikiliza malalamiko ya wananchi wakati alipotembelea visima vya maji katika shehia ya Welezo Unguja.

Alisema wananchi wanapata usumbufu mkubwa wa kupata huduma hiyo ambayo ni muhimu.

Alimtaka mkurugenzi wa mamlaka hiyo, kuwasimamia watendaji wa mamlaka hiyo ili kufanya kazi kwa ufanisi na kushughulikia tatizo la ukosefu wa maji.

Awali wananchi wa Shehia ya Welezo walisema wanakabiliwa na tatizo la ukosefu wa maji kwa muda mrefu.

Fatma Said Muhammed na Ameri Suleiman Hassan, ni miongoni mwa wananchi hao walisema wanashangazwa kuona visima vya ZAWA vilivyopo Welezo havitoi maji, lakini vinavyomilikiwa na watu binafsi vinatoa.

Aidha, wananchi hao waliiomba serikali kuwajengea barabara za ndani ili kuwaondolea changamoto wanazozipata wakati wanapofuata huduma za kijamii.

Walisema kukosekana kwa barabara hizo kunasababisha wafanyiwe vitendo vya kihalifu ikiwamo vitendo vya udhalilishaji.

Naye Mwakilishi wa Jimbo la Welezo, Hassan Khamis Hafidh, alisema kukosekana kwa huduma ya maji katika jimbo hilo kunatokana na miundombinu ya maji kuwa chakavu.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa ZAWA, Dk. Salha Muhammed, alisema visima saba vilivyopo Welezo, ni viwili pekee vinavyotoa maji.

Alisema visima hivyo vimeshindwa kutoa maji kwa sababu hawana mashine za kupandishia maji na wanahitaji Sh. milioni 300 kununulia mashine hizo na maji yapatikane.

Rais Mwinyi anaendelea na ziara yake hiyo katika Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja na anatarajiwa kumaliza ziara yake hiyo Julai 10, mwaka huu katika Mkoa wa Mjini Magharib na kuendelea na ziara yake Kisiwani Pemba.

## CCM: Tuna matumaini na jumuiya za chama

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

MJUMBE wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa, Hemed Suleiman Abdulla, amesema chama hicho kina matumaini makubwa na jumuiya za chama katika kufanikisha fikra, mikakati na mitazamo ya kuwaandaa vijana wake kushika nafasi za uongozi.

Mjumbe huyo wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa alieleza hayo wakati akifungua mkutano wa Baraza kuu la Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM), Mkoa wa Mjini uliofanyika mjini hapa.

Alisema wajibu wa wanachama wa CCM na Jumuiya zake zina jukumu la kuhakikisha chama hicho kinashinda katika chaguzi zote kama ilivyoelezwa ndani ya Katiba ya chama ibara ya 5(1) ikiwamo kushinda uchaguzi wa Serekali Kuu na Serikali za Mitaa kwa upande wa Tanzania Bara.

Aliwakumbusha wasimamizi wa jumuiya hiyo kutosahau wajibu wao wa kuwaandaa vijana ili wawe viongozi bora wa baadaye kupitia chama na serikali na kulinda, kutetea, pamoja na kushawishi vijana wengine kujiunga na chama hicho.

Alisema suala la serikali inayo tekeleza Ilani ya CCM kuwapa nafasi za uongozi vijana ni jambo lisilo epukika kwa kuzingatia mahitaji ya jamii na uendeshaji wa nchi kuhitaji vijana wenye weledi waliopikwa kupitia chama hicho.

Hemed aliwaeleza vijana wa UVCCM kwamba, CCM kupitia serikali zake zote mbili kimetoa nafasi nyingi za uongozi kwa vijana na marais wote wawili kupitia teuzi zao wameonyesha jinsi walivyojenga matumaini na kuwapa nafasi za uongozi vijana wanaotokana na chama hicho.

Makamu wa Pili wa Rais Hemed, alisema bado ipo haja ya kuwapa fursa vijana kupitia chaguzi mbalimbali hususani majimboni ili chama kiendelee kuwaanda vijana waweze kushika nafasi za uongozi.

Akisoma risala kwa niaba ya vijana hao wa UVCCM Mkoa wa Mjini Katibu wa Vijana wilaya ya Mjini, Ramadhani Abass Mcheju, alimweleza mgeni rasmi kuwa UVCCM ni chombo cha kuwaunganisha vijana pamoja kwa lengo la kuwapatia taaluma itakayowasaidia katika harakati za maisha yao ya kila siku. Alisema mkutano huo wa Baraza Kuu la Umoja wa Vijana Mkoa wa Mjini pia utajadili na kutathmini siku mia moja (100) za mama Samia tangu aingie madarakani ambapo wamefarijika sana na imani alioionyesha kwa kuwateua vijana kuwakabidhi dhamana ya Uongozi.

Katika risala yao vijana hao walimpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, kwa mkakati aliokuja nao wa kudhibiti mapato ya serikali na kuhakikisha anaziba mianya yote ambayo watumishi wasiokuwa waaminifu hutumia kwa kujinufaisha binafsi.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**HAJI AME HAMZA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **SUZUKI CARRY** yenye namba za usajili **T 282 DCE** chasis namba **DDSTT111800** engine namba **F6A87412369,** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa CONTROL NAMBA **9910823604407**

116349402

## KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJI

**THOBIAS JOSEPH KAVULA A**NATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 688BYW** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI TAARIFA YA POLISI KAG/ **BIH/RB/147104/2021**

116349602

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**STEPHEN JOSEPH NGOWI** Anatangaza kupotelewa kwa kadi yake ya gari aina yake **TOYOTA(Corolla)** yenye usajili Namba. **T 891 AKY,** Chassis namba.**KE726075792** na Engine namba.**4K6702118** Kwa yeyote atakae ona au kuokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Rb namba. **MOR/MOR/RB/339329/2021.**

116349802

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M 1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI 2**

**Katika mahakama ya mwanzo Mjini morogoro**

**Usimamizi wa mirathi 192/2021**

**Ombi la Gilbert Gilford Goda**
**Msimamizi wa mirathi wa marehemu Enock Gilford Goda**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja na kuhudhuria shaurini mnamo tarehe 22/7 /2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo kuwa msimamizi wa mirathi hiyo. Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.

116349902

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

Ndugu **JULIUS RAPHAEL DETEBA** anatangaza kupotelewa na Kadi za gari na tela zake zenye namba za usajili (1) **T.918ahq, T.432aks (2) T.821aeg, T.557ann (3) T.658age, T.608agq** yeyote atakaeziona atoe taarifa kituo chochote Cha polisi. **RB NO MOR/RUH/RB/335175/2021**

116350002

## KUPOTEA KWA CHETI



**PAULINA TLEMAI KWASLEMA**
Mwenye picha hapo juu anatangaza kwa kupotelewa kwa **full Academic Transcript** aliyopatiwa na chuo cha SUA mwaka 2020 kwa registration no.**EAB/D/2017/0035**
Kwa yeyote atakae ona au kuokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Rb namba.MAN/MBU/R**B/288950/2021.**

116350402

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**IN THE DISTRICT REGISTRY OF BUKOBA AT BUKOBA**

**LAND CASE APPLICATION NO 78/2020**
**(Arising from land application no 78/2010 Bukoba District land and Housing tribunal and land se no. 85/2010 of Kahororo WT)**

**GOZBERT KAHWA & 2 OTHER ............APPLICANT**

**VERSUS**

**MSAFIRI M. MALANJA .....................RESPONDENT**

**TO, MSAFIRI M. MALANJA**

**RE: NOTICE FOR DATE OF MENTION**

Wherease the above mentioned Applicants has lodged a case registered as land case application no 78/2020 against you at the High Court of Tanzania at Bukoba.
Take notice that the above said case has been scheduled for mention on 2nd day of August, 2021 at 09:00 am before Hon. J.M. MINDE DR. You are authorized to appear in person or through your Advocate.
Take further notice that in default of your appearance on that date and time for the said mention the case will proceed in your absence.
Give under my hand and seal of the court this 28th day of June, 2021.

J.M. MINDE
DEPUTY REGISTRAR
HIGH COURT OF TANZANIA
BUKOBA

116350602

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA**
**MAHALI DODOMA**
**MAOMBI NA.39 YA 2021**
**BAINA YA**
**RAFAEL CHIFNGO ....................................MUOMBAJI**
**DHIDI YA**
**JONATHAN CHIFUNGO..................MJIBU MAOMBI**

**KWA: JONATHAN CHIFUNGO**

**POPOTE ULIPO**

**YAH: KUITWA SHAURINI**
**KWA KUWA:** muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya Maombi ambayo yanapatikana katika Baraza hili.
**KWA HIYO** unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili wewe binafsi, Wakili au mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 21. 07. 2021 saa 3.00 asubuhi. kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.

**ANGALIZO:** kama hukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu. Baraza likidhibitisha kuwa umepokea Hati ya wito, Baraza linaweza kutoa hukumu dhidi yako.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na lakiri/Muhuri wa baraza hii leo tarehe 02 ya mwezi wa Julai,2021.

11635122

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

NICOLAUS PETER MUSHI anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya BOKSA yenye namba za usajili MC 337 ASZ,yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa DAR/OST/R-B/337846/2021

116351502

Uza,
Chenye Thamani Kubwa
Kwa Kutangaza Nasi Kwa
Bei Poa
Tupigie 0782253676

WAUNGWANA AUCTION MART LTD
P. O. BOX 75965 DAR ES SALAAM
Mob: +255713077474, 0717023338
E-mail: waungwana2017@gmail.com

## NOTISI/TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kwa mamlaka tuliyopewa na **LETSHEGO BANK (T) LTD** tunauza kwa njia ya mnada wa hadhara Shule ambayo ni mali za mdaiwa / mdhamini iliyowekwa kama dhamana ya mkopo ambapo mteja husika ameshindwa kulipa mkopo wake kwa mujibu wa mikataba husika. Minada yote itafanyika kuanzia saa 4 asubuhi na kuendelea.

| S/N | JINA LA MTEJA | JINA LA MDHAMINI | AINA YA DHAMANA | DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | ANGANILE ANDREW | ANGANILE ANDREW | SHULE PLOT NO.305 BLOCK D MBALIZI | MBALIZI NJIA YA KWENDA CHUNYA | 23/07/2021 |

**MASHARTI YA MNADA**
. Ukaguzi unaruhusiwa mara usomapo gazeti hili
. Mnunuzi atalazimika kulipa malipo ya 25% ya fedha taslimu papo hapo na 75% kwa baada ya siku 14 toka siku ya mnada kufanyika na ukishindwa kulipa mnada utarudiwa na fedha ulizolipa hazitarudiwa
. Gharama zozote ikiwemo za kubadilisha taarifa za nyaraka za umiliki ni za mnunuzi.

**Kwa mawasiliano 0713 077474/0658370615**
**Waungwana auction mart limited**
**WOTE MNAKARIBISHWA**

116351602

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI
INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042,
DAR ES SALAAM. MOB:
+255 - 0782253676

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Zuma aanza kutumikia kifungo gerezani

**Kwa-Zulu-Natal,** AFRIKA KUSINI

ALIYEKUWA Rais wa zamani wa Afrika Kusini, Jacob Zuma, amejisalimisha mwenyewe Polisi na kuanza kutumikia kifungo cha miezi 15 alichohukumiwa na Mahakama ya Katiba, kwa kosa la kutotii wito wa mahakama.

Polisi, Afrika Kusini imethibitisha, baada ya kujisalimisha mwenyewe, ikiwa imepita wiki moja tangu alipokutwa na hatia ya kuidharau mahakama kufuatia kesi yake ya ufisadi na kuhukumiwa kifungo cha miezi 15 gerezani.

Usiku wa kuamkia jana umekuwa ni wa kwanza na gerezani kwa Zuma, baada ya kujisalimisha mwenyewe kwa mamlaka husika.

Msemaji wa Polisi Lirandzu Themba amethibitisha kuwa Zuma yuko chini ya ulinzi wa polisi baada ya kujisalimisha.

Dakika chache tu kabla ya muda wa mwisho aliyopewa na korti kujisalimisha kwa hiari kabla ya polisi kumkamata, Zuma aliondoka nyumbani kwake Nkandla akisindikizwa na msafara wa magari.

Kwa mujibu wa taarifa zilizotolewa, rais huyo mstaafu ameamua kutii agizo la kufungwa kwake.

Baada ya kufikia makubaliano ya kujisalimisha kwake na ujumbe wa Polisi uliofika nyumbani kwake mapema juzi, Zuma, akisindikizwa na walinzi wake alienda katika gereza lililokaribu na nyumbani kwake katika jimbo la Kwa-Zulu-Natal.

Baadhi ya wafuasi wake waliokuwa wamekusanyika nje ya nyumba yake walielezea kutofurahishwa na kiongozi wao huyo kuhukumiwa kifungo gerezani.

Awali polisi ilitoa onyo la kutaka kumkamata rais huyo mstaafu mwenye umri wa miaka 79, iwapo hatajisalimisha mwenyewe, ifikapo usiku wa jana.

Zuma mwanzoni mwa wiki hii alitaja hukumu hiyo kama ya kifo kutokana na umri wake.

Alishtakiwa kwa tuhuma za ufisadi katika kipindi cha miaka tisa ya uongozi wake madarakani. Tuhuma ambazo mwenyewe alizikana na kusema kuwa ni mhanga wa kisiasa.

Wakfu wa Zuma Foundation uliandika katika mtandao wake wa Twitter kuwa kiongozi huyo ameamua kuheshimu agizo la korti na kwamba alikuwa njiani kuelekea katika kituo cha polisi cha wilaya ya Kwa Zulu-Natal.

Katika taarifa nyingine, mamlaka ya magereza ilisema Zuma amefikishwa kwenye kituo cha mamlaka ya magereza, umbali wa kilomita 175 kutoka makazi yake ya mji wa Nkandla.

Jibu la viongozi kwa mwenendo wa Zuma kukataa kutoa ushirikiano katika uchunguzi baada ya miaka kadhaa ya madai ya ufisadi na uovu, imeonekana ni mtihani kwa Afrika Kusini baada ya kipindi cha utawala wa ubaguzi wa rangi, kuweza kutekeleza sheria.

Zuma alikanusha kwamba kulikuwapo ufisadi uliokithiri chini ya uongozi wake, na Jumapili, alionyesha kitendo cha kukaidi, kwa kulinganisha majaji waliomuhukumu na wazungu walio wachache waliotawala enzi za utawala wa ubaguzi wa rangi, ambao aliwahi kuwapiga vita.

Binti yake Dudu Zuma-Sambudla, kwenye ukurasa wake wa Twitter, aliandika kuwa, baba yake alikuwa njiani kwenda jela, lakini alikuwa katika hali nzuri.

Hii ndio mara ya kwanza raia wa Afrika Kusini wanashuhudia rais wao wa zamani akifungwa jela.

Zuma aliwahi kufungwa jela wakati wa mapambano dhidi ya ubaguzi wa rangi nchini mwake.

Mwanasiasa huyo mwenye sifa ya ucheshi, aliondolewa madarakani na Chama cha ANC baada ya kudaiwa kujihusisha na ufisadi, na nafasi yake kuchukuliwa na rais wa sasa Cyril Ramaphosa.

Rais huyo wa zamani alikabiliwa na mashtaka 16 ya ufisadi, kwa kuhusika na ununuzi wa silaha kutoka kampuni za kuuza silaha barani Ulaya.

**BBC/DW/VOA/RFI**

# Wanne wauawa shutuma mauaji rais

**Port-au-Prince,** HAITI

POLISI Haiti wamewaua watu wanne, wanaoshukiwa kuhusika na kifo cha rais wa nchi hiyo Jovenel Moise siku ya Jumatano.

Wengine wawili wametiwa mbaroni wakati viongozi mbalimbali duniani wakilaani kuuawa kwa kiongozi wa nchi hiyo ya eneo la Caribbean.

Mpaka sasa haijafahamika wauaji wa rais huyo walikuwa na nia gani, na ni kina nani.

Imeripotiwa kuwa wauaji hao walikuwa wanazungumza lugha ya Kiingereza na Kihispaniola.

Mkuu wa Jeshi la Polisi Leon Charles alisema msako unaendelea kuwatafuta washukiwa zaidi wa mauaji hayo na kwamba polisi wanawatafuta wauaji.

Marekani ilisema tukio hilo la kusikitisha, linapaswa kuwaunganisha raia wa nchi hiyo.

“Baada ya tukio hilo la kusikitisha sisi kama viongozi, tunapaswa kuwa na njia ya kuja pamoja, kwa hivyo nafikiri kwa sasa ni kiongozi kukaa na kila mmoja na kutulia suala hilo la kusikitisha kwa maslahi ya nchi na sio kuigawa nchi zaidi.”

Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, limelaani mauaji ya kiongozi huyo na kutaka wale wote waliohusika kukamatwa na kuchukuliwa hatua.

Waziri Mkuu, Claude Joseph alitangaza hali ya dharura na kueleza kuwa kwa sasa yeye ndiye anayeongoza nchi hiyo wakati huu mitaa ya jiji kuu Port-au-Prince, ikisalia bila watu na uwanja wa ndege kufungwa.

**RFI**



Msafara wa magari uliombeba aliyekuwa Rais wa Afrika Kusini, Jacob Zuma wakati akipelekwa gerezani jana. PICHA: BBC

# Sudan Kusini yakabiliwa na njaa

**Juba,** SUDAN KUSINI

SUDAN Kusini inakabiliwa na uhaba wa chakula huku ikitimiza miaka 10 baada ya uhuru.

Ripoti kutoka Shirika la Chakula Duniani (WFP), iliyotolewa mwezi uliopita inasema kuwa asilimia 60 ya wakazi milioni 7.2 wa Sudan Kusini wanakabiliwa na ukosefu wa usalama wa chakula kwenye robo ya kwanza ya mwaka huu.

Kulingana na Mwenyekiti wa Taasisi ya kiuchumi ya Sudan Kusini, Laku Likang, taifa hilo linaagiza asilimia 80 ya chakula kutoka mataifa ya nje.

Vyakula kama mboga na nyanya miongoni mwa vingine kwa mfano huagizwa kutoka Uganda.

Wakati akizungumza kipindi cha VOA cha South Sudan in Focus, Lukang alisema kwamba tangu taifa hilo lijipatie uhuru wake, bado halijaweza kubuni viwanda vya kutengeneza bidhaa kama vile mafuta ya kupikia au hata sukari.

Aliongeza kusema kuwa licha ya taifa hilo kuwa na mafuta ghafi, fedha zinazopatikana zinahitajika kununua vifaa muhimu vya kilimo kama matrekta ili kuongeza uzalishaji wa chakula.

**VOA**

# Bonucci: Mechi ya Hispania ilikuwa ngumu



**LONDON,** England

MLINZI wa Italia, Leonardo Bonucci amekiri mchezo dhidi ya Hispania ulikuwa mgumu zaidi kuwahi kucheza wakati Azzurri ilijihakikishia nafasi ya kutinga fainali ya Euro 2020.

Kikosi cha Bonucci kiliizidi Hispania kwa mikwaju ya penalti, na kupata nafasi ya kucheza fainali dhidi ya England.

"Huu ni mchezo mgumu zaidi kuwahi kucheza. Nawapongeza Hispania kwa kile walichoonyesha, lakini kwa mara nyingine Italia hii ilionyesha moyo, dhamira na uwezo wa kushinikiza wakati mgumu na bahati ya penalti ilitupatia ushindi," alisema Bonucci akiiambia RAI Sport.

"Ushindi unaoteseka ni wa kufurahisha zaidi kila wakati."

"Sasa kuna sentimita moja zaidi ya kwenda. Sentimita moja tu, "aliongeza." Ni ajabu tunachofanya, lakini hatupaswi kuhisi kuridhika. Tuko fainali. Ni katika siku tano, na tunahitaji njaa sawa na roho ya kujitolea kuleta kombe hili nyumbani baada ya miaka mingi.

# Griezmann aomba radhi kwa ubaguzi



**PARIS,** Ufaransa

NYOTA wa Barcelona, Antoine Griezmann ameripotiwa ameomba msamaha kwa mabosi wanaoifadhili Barcelona baada ya utani aliofanya uliotafsiriwa kama ubaguzi.

Griezmann na mwenzake Ousmane Dembélé wametokea katika video iliyozua utata ambayo walionekana wakiwatania wafanyakazi wa Kijapani.

Kwa mujibu wa staa huyo, video hiyo ambayo ilivuma kwenye mitandao ya kijamii ilitafsiriwa vibaya kwa kuhusishwa na ubaguzi.

Baada ya kuonekana kwa video hiyo Griezmann aliomba msamaha mapema kupitia ukurasa wake wa Twitter.

"Wakati wote nimekuwa kipaumbele kupambana na kila aina ya ubaguzi. Kwa siku za hivi karibuni, baadhi ya watu wameamua kunitangazia kile ambacho si mimi. Ninakanusha madai juu yangu na naomba msamaha ikiwa niliwaudhi marafiki zangu wa Japan," aliandika Griezmann.

Licha ya chapisho la Griezmann, Mkurugenzi wa Japanese ambao ni miongoni mwa wafadhili wa Barcelona Rakuten, Hiroshi Mikitani naye pia alichapisha akidai kuwa atafuatilia kwa ukaribu zaidi kupata majibu kutoka klabuni hapo juu ya suala hilo.

Taarifa zingine zinasema kuwa Griezmann tayari pia amefanya mawasiliano na mkurugenzi huyo kuomba msamaha juu ya kilichotokea.

# Messi aionya Argentina kuhusu Neymar



**RIO DE JANEIRO,** Brazil

NYOTA wa Argentina, Lionel Messi amewatumia ujumbe wa onyo wachezaji wenzake wa Timu ya Taifa juu ya Neymar kuelekea fainali ya Copa America.

Messi na Argentina walipenya kuingia kwenye fainali ya Copa America 2020 baada ya kushinda kwa penalti dhidi ya Colombia.

Argentina walianza kwa kuwachapa bao la mapema Colombia kupitia Lauturo Martinez kabla ya Luis Diaz kusawazisha na kulazimisha wacheze hadi muda wa nyongeza na hatimaye mashuti ya penalti.

Kufika fainali kwa Argentina ni nafasi ya Messi kushinda taji kubwa akiwa na timu yake ya taifa, lakini kibarua kilichopo ni kuruka kiunzi cha Brazil ambao wapo pamoja na Neymar Jr.

Kuelekea fainali Jumapili hii, Messi amewaambia Argentina kuwa Brazil wakiwa na Neymar watakuwa wagumu sana na wanahitaji kujiandaa kwa sababu ya hilo.

"Brazili wakiwa na Neymar watakuwa wagumu sana, tunamfahamu uwezo wake na kile anachoweza kukifanya binafsi," alisema Messi akinukuliwa na BBC Sport.

"Nina amini mchezo utakuwa mgumu sana kwa upande wetu, lakini lazima tuwe makini na tuweze kushinda."

## HABARI MICHEZO




# Liverpool wajitosa kwa Mbappe

**LIVERPOO,** England

LIVERPOOL inaongoza kwenye mbio za kuwania kumsajili nyota wa Paris Saint-Germain, Kylian Mbappe, kwa mujibu wa RMC.

Majaliwa ya Mbappe pale kwenye jiji la Paris yametawala vichwa vya vyombo vya habari kwa siku za hivi karibuni.

Mbappe amekuwa akitajwa kuwaniwa na Real Madrid kwa muda mrefu, baada ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 kuweka wazi kwamba hana mpango wa kuongeza mkataba pale PSG.

Mkataba wa Mbappe pale PSG unamalizika mwishoni mwa msimu wa 2021-22 na amekuwa ahusishwa sana kujiunga na miamba wa LaLiga, Real Madrid.

PSG bado hawajaweza kumshawishi Mbappe kusaini mkataba mpya na nyota huyo wiki iliyopita alinukuliwa akisema hana mpango wa kufanya hivyo, kwani anataka kuondoka na kwenda kutafuta changamoto mpya.

Na sasa kwa mujibu wa ripoti ya RMC ya jana Jumatatu, Liverpool ndio wanaongoza katika mbio za kuwania kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa ambaye alikosa penalti dhidi ya Uswisi na timu yake kutolewa kwenye Euro 2020 hatua ya 16.

Ripoti hiyo imebainisha kuwa, Liverpool wanajiandaa kutuma ofa rasmi kwa PSG kwa ajili ya kumsajili kipindi cha dirisha kubwa la majira ya joto.

# Barca yamweka Coutinho sokoni




**BARCELONA,** Hispania

KLABU ya Barcelona imeripotiwa ipo tayari kukubali ofa ya pauni milioni 20 kwa ajili ya kumwachia kiungo wake, Philippe Coutinho.

Licha ya kuondoka Liverpool kwa pauni milioni 142 Januari 2018, Coutinho ameshindwa kutamba huko Camp Nou, na kumweka mchezaji huyo mahali ambapo analazimishwa kuondoka klabu hapo.

Maofisa wa klabu wanataka kumuuza Coutinho mwenye umri wa miaka 29 ili kupunguza gharama kwenye bili yao ya mshahara, lakini ilishindikana kutokana na Mbrazil huyo kupata jeraha la goti tangu Desemba, mwaka jana.

Barcelona wanahitaji fedha ili kumbakiza Lionel Messi ambaye mkataba wake umekwisha klabuni hapo, klabu hiyo ipo tayari kupokea pauni milioni 20 kwa mchezaji huyo katika msimu huu wa joto.

Barcelona tayari wamemruhusu Francisco Trincao kuhamia Wolverhampton Wanderers kwa mkopo, wakati Samuel Umtiti na Miralem Pjanic wamepewa uhamisho wa bure.

# Deschamps hali tete Ufaransa



**PARIS,** Ufaransa

DIDIER Deschamps atafanya mazungumzo na Rais wa Shirikisho la Soka la Ufaransa (FFF), Noel Le Graet wiki chache zijazo baada ya kikosi hicho kuondolewa kwenye michuano ya Euro 2020.

Kabla ya kuanza kwa michuano hiyo, Ufaransa ilikuwa ikipewa nafasi kubwa ya kutwaa taji hilo na iliongoza kundi lake lililokuwa na timu za Ureno, Ujerumani na Hungary, na ikatolewa hatua ya 16 kwa changamoto ya mikwaju ya penalti na Uswisi.

Hiyo ilikuwa ni mara ya kwanza tangu michuano ya Kombe la Dunia mwaka 2010 kwa Les Blues hao kushindwa kufuzu robo fainali kwenye mashindano makubwa.

Kuondolewa mapema kwa Ufaransa kumezua maswali mengi kuhusu majaliwa ya Deschamps, huku Zinedine Zidane akitajwa kuhusishwa na kazi hiyo tangu alipoondoka Real Madrid, Mei mwaka huu.

Mkataba wa sasa wa Deschamps unamalizika baada ya Kombe la Dunia mwaka 2022 nchini Qatar tangu alipochukua mikoba hiyo mwaka 2012, akibeba Kombe la Dunia mwaka 2018 na kutinga fainali ya Euro 2016.

La Great alinukuliwa wiki iliyopita akisema kwamba, kocha huyo mwenye umri wa miaka 52 nafasi yake haipo shakani, lakini kigogo huyo wa FFF anapanga kukutana na Deschamps kwa siku chache zinazokuja.

"Tutakutana wiki ijayo. Mara zote naacha siku 10 zipite," La Graet aliiambia Telefoot.

"Tutakutana ofisini kule Guingamp na tutakuwa na siku nzima pamoja. Kila mmoja anatakiwa kufikiri kuhusu nini kipo sawa na kipi hakipo sawa."

Alipoulizwa kuhusu kauli yake ya hivi karibuni juu ya majaliwa ya kazi ya Deschamps, La Graet alisema: "Sikusema hivyo. Nilisema tutakuwa na majadiliano. Tutazungumza kuhusu nini kilichokwenda vibaya."

HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# NI ITALIA VS ENGLAND FAINALI ZA EURO 2020

●●● Timu zote zimetinga hatua hiyo zikiwa na rekodi ya kutoruhusu nyavu zake kutingishwa...

**LONDON,** England

TIMU ya Taifa ya England imefanikiwa kutinga katika hatua ya fainali ya michuano ya Euro 2020, baada ya kuwafunga Denmark mabao 2-1, kwenye mchezo wa nusu fainali uliopigwa kwa dakika 120, katika dimba la Wembley, juzi.

Denmark walikuwa wa kwanza kufunga bao dakika ya 30 kwa mpira wa adhabu uliopigwa na mshambuliaji wa timu hiyo, Mikkel Damsgaard, kabla ya England kusawazisha bao hilo baada ya nahodha wa Denmark, Simon KJaer kujifunga kutokana na krosi iliyopigwa na winga wa England, Bukayo Saka. Hadi dakika 90 zinamalizika, timu hizo zilikuwa zimefungana bao 1-1, lakini nahodha wa England, Harry Kane aliifungia timu yake bao la pili dakika ya 104, katika dakika 30 za nyongeza.

**Italia ilitinga hatua ya fainali baada ya kuifunga Hispania kwa mikwaju ya penalti, katika mchezo wa nusu fainali uliochezwa Wembley.**

Italia itacheza na England, Julai 11, mwaka huu, kwenye uwanja wa taifa wa England, Wembley, huku timu hizo zikiwa na rekodi nzuri ya kutoruhusu mabao mengi kwenye michuano hiyo.

Italia wameruhusu mabao matatu pekee katika mechi tano walizocheza, huku England ikiwa na rekodi ya kucheza michezo mitano na kuruhusu bao moja pekee.

## KWA UFUPI

**RONALDO KIMEELEWEKA**

WAKALA wa Cristiano Ronaldo, Jorge Mendes anafanyia kazi mpango wa kuongezwa mkataba kwa nyota huyo ili abakie Juventus kwa mwaka mmoja zaidi.(***Sky Sport Italia***)

**UNITED MAMBO MAGUMU**

UWEZEKANO wa Manchester United kumsajili Cristiano Ronaldo kipindi hiki cha majira ya joto ni mdogo, kwa mujibu wa wakala wake, Jorgr Mendes. (***Gazzetta dello Sport***)

**UMTITI, PJANIC KUUZWA**

BARCELONA wako tayari kukatisha mikataba ya wachezaji wake, Miralem Pjanic mwenye umri wa miaka 31 na mlinzi wa Ufaransa, Samuel Umtiti (27), ambao wanaonekana hawako kwenye mipango ya kocha, Ronald Koeman. (***Goal***)

**PJANIC ANUKIA SPURS**

NYOTA wa Barcelona, Miralem Pjanic mwenye umri wa miaka 31 anahusishwa na uhamisho wa kuelekea Tottenham Hotspur. (***Express***)

**INSIGNE AGEUKA LULU**

KLABU za Tottenham na Barcelona wanamwania nahodha wa Napoli, Lorenzo Insigne mwenye umri wa miaka 30, ambaye ameng'ara katika michuano ya Euro 2020. (***Corriere dello Sport***)

**COUTINHO NJIA MOJA**

BARCELONA wako tayari kupokea ada kiduchu kwa ajili ya kiungo wake Mbrazil Philippe Coutinho kuliko ile waliyoilipa Liverpool wakati nyota huyo mwenye umri wa miaka 29 alipojiunga na wakali hao wa La Liga, thamani yake inaendelea kushuka.(***Sky Sport***)

**RYAN ANUKIA SOCIEDAD**

GOLIKIPA wa Brighton, Mat Ryan mwenye umri wa miaka 29, ambaye aliichezea Arsenal kwa mkopo msimu uliopita anakaribia kutua Real Sociedad. (***Sky Sports***)

**WILLOCK ATAJWA NEWCASTLE**

MLINZI wa zamani wa Newcastle, Steve Howey anasema klabu hiyo lazima imsajili kiungo Joe Willock mwenye umri wa miaka 21, msimu huu au wawe katika hatari ya kumkosa kabisa huko mbeleni, kwa sababu ya vita ya bei ya nyota huyo wa Arsenal ni kubwa. (***Chronicle***)

**MENDY AKARIBIA INTER**

MLINZI wa kushoto wa Manchester City, Benjamin Mendy mwenye umri wa miaka 26, anatajwa kuwa kwenye orodha ya nyota wanaotakiwa na Inter Milan. (***Manchester Evening News***)

**UNITED YAMTAKA KOUNDE**

KLABU ya Manchester United itamgeukia mlinzi wa Sevilla na Ufaransa, Jules Kounde mwenye umri wa miaka 22, kama mbadala wa Raphael Varane (28), endapo watashindwa kumsajili mlinzi huyo kutoka Real Madrid. (***AS***)

**FIRPO SAFI LEEDS**

MLINZI wa kushoto wa Barcelona, Junior Firpo mwenye umri wa miaka 24, anakaribia kukamilisha uhamisho wake wa kudumu kujiunga na Leeds United. (***The Athletic - subscription required***)

## Yanga yapigwa faini milioni 3.8

**Na Mwandishi Wetu**

KLABU ya Yanga itatakiwa kulipa faini ya Sh. milioni tatu kutokana na kubainika kufanya makosa manne katika siku ya mchezo marudiano wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya watani zao Simba, ambao ulimalizika kwa wao kupata ushindi wa bao 1-0, imefahamika.

Taarifa iliyotolewa na Idara ya Mawasiliano ya Bodi ya Ligi Kuu (TPLB), jana ilisema Yanga imepewa adhabu hiyo baada ya kutumia mageti ya Uwanja wa Uhuru kuingia kwenye Uwanja wa Benjamini Mkapa badala ya mlango maalumu unaotakiwa na timu zote.

Yanga pia ilitumia chumba cha wanahabari badala ya mlango maalumu unaofahamika na iliingia uwanjani kupasha mwili kwa kutumia mlango wa geti namba B ambao haukupangwa kutumika kwa namna yoyote.

Klabu hiyo pia imeadhibiwa kwa kutumia chumba cha wafanya usafi wa uwanja kubadilisha nguo badala ya chumba maalumu kinachofahamika.

"Pia Yanga inatakiwa kulipa kiasi cha Sh. 850,000 ikiwa ni gharama ya ukarabati wa mageti yaliyovunjwa wakati wakiingia uwanjani pamoja na makufuli ya uwanja wa Benjamin Mkapa yaliyoharibiwa katika tukio hilo," iliongeza sehemu ya taarifa.

Wakati huo huo Ruvu Shooting imepewa onyo kali kwa kosa la mchezaji wake, Samson Kwakwala kuvaa jezi yenye namba 71 mgongoni katika mchezo wao namba 287 dhidi ya Polisi Tanzania ambayo ni kinyume na taratibu zilizowekwa.

## Klabu ya Mazoezi Shinyanga yanunua mitungi ya Oksijeni

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

KLABU ya Mazoezi ya Polisi Jamii (PJFCS), ambayo ipo chini ya Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga, imetoa msaada wa mitungi 16 ya Oksijeni katika Hospitali ya Rufani mkoani humo, ili kusaidia wagonjwa wenye changamoto ya upumuaji.

Mwenyekiti wa klabu hiyo, Sadick Kibira alisema waliamua kununua mitungi hiyo baada ya kukusanya kiasi cha Sh. 928,000 kutoka kwa kila mwanachama wa klabu hiyo ili kusaidia wagonjwa wenye changamoto hiyo. Kibira alisema kila mwaka wakati wa sherehe za Sabasaba, klabu hiyo huadhimisha kwa kutoa misaada mbalimbali kwa wahitaji pamoja na kuchangia damu, ambapo kwa mwaka huu wameamua kutoa msaada huo.

"Tumetoa mitungi hii ya hewa ya oksijeni 16 katika Hospitali ya Rufani mkoani Shinyanga na kuchangia damu, ambapo mitungi hii itasaidia kwa kiasi kikubwa kuhudumia wagonjwa wenye changamoto ya upumuaji," alisema Kibira.

Naye Kaimu Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Shinyanga, Dk. Mfaume Salum, alisema msaada waliopokea umesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza changamoto ya upungufu wa mitungi hospitalini hapo.

Kwa upande wake Mnadhimu wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Shinyanga, Joseph Paul akizungumza kwa niaba ya Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga George Kyando, alipongeza klabu hiyo kwa kutoa msaada huo na kutoa wito kwa wadau wengine waige mfano huo.

# NDEMLA, GADIEL KAMILI KUIKABILI COASTAL UNION

**Na Saada Akida**

BAADA ya timu yake kuwa katika nafasi nzuri ya kutetea ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa mara ya nne mfululizo, Kocha Mkuu wa Simba, Didier Gomes amesema atawapumzisha baadhi ya wachezaji wake nyota na kuwapa nafasi wengine waliosotea benchi akiwamo kiungo, Said Ndemla.

Juzi usiku Simba iliibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya KMC FC na kufikisha pointi 76 ambazo zinaweza kufikiwa na Yanga tu, hivyo wanahitaji pointi moja tu kutangazwa mabingwa wapya wa msimu wa 2022/21.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Gomes alisema msimu huu ulikuwa mrefu na wachezaji wake walipambana kwa kiwango kikubwa kufanikisha wanatetea ubingwa na sasa atatumia nyota ambao hawajacheza kwa muda mrefu katika mechi zao tatu za ligi zilizosalia. Gomes aliwataja wachezaji hao ni pamoja na Ndemla, Miraji Athumani, Gadiel Michael na David Kameta ambao wanafanya vizuri katika mazoezi lakini kutokana na ukubwa wa kikosi wameshindwa kupata nafasi.

"Tunashukuru tumefanikiwa kutetea ubingwa wetu, nafikiria kuwapumzisha baadhi ya wachezaji ambao wametumika zaidi na kuwapa nafasi wengine, ligi ilikuwa ndefu na mechi zilikuwa karibu na pia tunajiandaa na mchezo wa fainali ya FA."

"Katika mechi tatu za ligi zilizobaki tutawapa nafasi wachezaji ambao hatukuwatumia sana. Simba ni familia, ukipanga kikosi bado unakuwa na wachezaji 10 ambao ni bora, lakini wanakosa nafasi hivyo ni wakati wao huu," alisema Gomes. Kuhusu mchezo wao dhidi ya KMC, kocha huyo alisema anajivunia sana kiwango kilichoonyeshwa na wachezaji wake kwa sababu walifuata maagizo aliyowapa walipokuwa katika mazoezi.

"Niliwapa maelekezo wachezaji wangu kuhakikisha KMC kutocheza mpira wao na kuharibu mbinu za wapinzani wao hao na kufanikiwa, najivunia sana jinsi wachezaji wanavyopambana ukiangalia safu ya ushambuliaji iko imara, Mugalu kwangu ni straika bora sana, lakini wachezaji wote wa mbele wanacheza vizuri, kitu kizuri kwa John Bocco ni mpambanaji sana," Gomes aliongeza.

Naye Kocha Msaidizi wa KMC, Habib Kondo alisema mipango ya timu yake katika mechi hiyo "ilifeli" na kusababishwa kuadhibiwa na Simba.

"Tumefeli kila sehemu katika 'Game plan' yetu na tulipaswa kuadhibiwa, hatukutengeneza nafasi yoyote ya kufunga, hii inaonyesha jinsi gani ligi inaushindani, kila mmoja anakuja na mipango yake, tunakubaliana na matokeo."

"Simba ilikuwa bora zaidi yetu walituzidi kila kitu, hatukutengeneza hata nafasi moja kwenye mchezo wa leo, tunaenda kujipanga kwa ajili ya mechi zilizosalia," alisema Kondo.



Kikosi cha mabingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania Bara, Simba Queens ya jijini Dar es Salaam kikiwa kwenye mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mashindano ya Kanda ya Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), yatakayofanyika baadaye mwezi huu huko Nairobi nchini Kenya. **PICHA: SIMBA SC**

# Kaseja: Simba ni timu bora

**Na Adam Fungamwango**

NAHODHA wa KMC FC, Juma Kaseja amesema Simba ni timu bora na ina wachezaji wenye uwezo wa hali ya juu, hivyo walizidiwa katika mchezo wao wa Ligi Kuu Tanzania Bara uliochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam juzi.

Katika mechi hiyo, Simba iliibuka na ushindi wa mabao 2-0 na kufikisha pointi 76 huku KMC ikibakia na pointi zake 42.

Kaseja, golikipa wa zamani wa Moro United, Simba, Yanga na Kagera Sugar alisema timu yake ilizidiwa zaidi katika kipindi cha kwanza ambacho mabingwa hao watetezi walipata mashambulizi mbalimbali.

Golikipa huyo aliongeza kipindi cha pili timu yake iliimarika baada ya kuyaona makosa yao na ilionyesha mchezo mzuri, ingawa walikutana na ugumu wa wachezaji wa Simba ambao tayari walikuwa wameshapata mabao mawili mkononi.

"Mechi tuliikosea kipindi cha kwanza. Hatukucheza kama ilivyopaswa tucheze. Kwa sababu tulicheza na timu bora yenye wachezaji wenye uwezo wakatuadhibu. Kipindi cha pili baada ya kuyaona makosa yetu tulijirekebisha, lakini tayari tulikuwa nyuma kwa magoli mawili. Na timu kama Simba ikishakutangulia kwa mabao hayo, mechi inakuwa ngumu sana," alisema Kaseja.

KMC imepoteza mechi zote mbili msimu huu dhidi ya Simba, katika mechi ya mzunguko wa kwanza ilichapwa bao 1-0 ambalo lilifungwa kwa mkwaju wa penalti na Meddie Kagere kwenye dakika za majeruhi za mchezo, Desemba 16 mwaka jana na juzi usiku, mabao yote mawili yaliwekwa wavuni na Mkongomani Chris Mugalu.

KMC imebakisha mechi mbili na hata ikishinda itafikisha pointi 48, hivyo matumaini na kumaliza kwenye nafasi nne za juu msimu huu yamepotea kwa sababu nafasi ya nne inashikwa na Biashara United yenye pointi 49 na yenyewe pia ina michezo miwili mkononi.

# Michezo

Ijumaa Julai 9, 2021

Nipashe




## BARCA YAMWEKA COUTINHO SOKONI

HABARI UK 21




Kiungo wa Simba, Clatous Chama (kulia), akijiandaa kumtoka beki wa KMC FC, Andrew Vincent 'Dante' katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam juzi usiku. Simba ilishinda mabao 2-0. PICHA: SIMBA SC

## SIMBA MIPANGO YOTE ITATIMIA

**Na Saada Akida**

NYOTA wa Simba, Bernard Morrison amesema akili na nguvu zao zote wanazielekeza zaidi katika michezo mitatu ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyobakia ikiwamo dhidi ya Azam FC na kuiweka 'kando' mechi ya fainali ya Kombe la FA ambayo watakutana na Yanga Julai 25, mwaka huu mkoani Kigoma.

Simba itacheza dhidi ya Coastal Union keshokutwa Jumapili halafu itakutana na Azam FC Julai 14, mwaka huu na siku nne baadaye itafunga pazia la msimu huu kwa kuwakaribisha Namungo FC kwenye dimba la Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Morrison aliliambia gazeti hili alisema wanajipanga kuhakikisha wanashinda mechi hizo zilizobakia na kumaliza msimu kwa furaha ili kuung'arisha ubingwa wa ligi hiyo ambao tayari uko 'mikononi' mwao.

"Tumefanikiwa kupata pointi tatu dhidi ya KMC FC na kujihakikishia ubingwa, ila bado tunahitaji kupata matokeo katika mechi tatu zilizobaki ambazo ni ngumu kwa sababu tunaelekea ukingoni mwa ligi na kila mmoja anahitaji kupata matokeo mazuri."

"Kila mechi tunapomaliza ni maandalizi ya mechi ijayo, sasa tumemaliza dhidi ya KMC FC na tunaanza mikakati ya kuwakabili Coastal Union, tukimaliza mechi hizo tutakuja kuizungumzia fainali," alisema Morrison.

Nyota huyo amewaomba radhi mashabiki wa Simba kutokana na timu yao kushindwa kupata matokeo mazuri walipocheza dhidi ya Yanga Jumamosi iliyopita.

Morrison ambaye alicheza dk 90 katika mchezo huo ambao Yanga waliondoka na ushindi wa bao 1-0, lililofungwa na Zawadi Mauya alisema walipambana kusaka ushindi lakini bahati haikuwa siku hiyo na wanaamini matokeo waliyopata yaliwaumiza mashabiki wao.

Simba inaongeza katika msimamo wa ligi ikiwa na pointi 76 ikifuatiwa na Yanga yenye pointi 70 wakati Azam FC yenye pointi 70 huku Mwadui FC ya Shinyanga yenye pointi 19 imeshashuka daraja.

# Azam yaimwagia Yanga mabilioni

## Pia kampuni hiyo yatangaza kuwapa bonasi nono msimu ujao endapo itamaliza katika...

**Na Saada Akida**

IKIWA ni mwezi mmoja umepita baada ya Azam Media kusaini mkataba mnono na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kampuni hiyo imeingia mkataba mwingine wa miaka 10 na Klabu ya Yanga wenye thamani ya Sh. bilioni 41,imefahamika.

Mkataba huo ambao unahusiana na uchakataji maudhui (Media Partnership) umesainiwa na viongozi wawili wa juu ambao ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa Azam Media, Tido Mhando na Yanga iliwakilishwa na Mwenyekiti wake, Mshindo Msolla.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Mhando alisema baada ya makato ya kodi, Yanga itapokea kiasi cha Sh. bilioni 34.8 na lengo kubwa la kusaini mkataba huo ni kuendelea kuimarisha ushirikiano na klabu hiyo inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara.

**Mhando alisema mkataba huo utaifanya Azam TV, kurusha chaneli ya Yanga TV, matukio yote ya Yanga ikiwamo mechi za kirafiki, kimataifa na shughuli nyingine mbalimbali zitakazosimamiwa na klabu hiyo zinazolenga maendeleo.**

"Miaka mingi Azam Media walikuwa karibu na Yanga, kwa sasa tumeimarisha ukaribu wetu kwa kuhakikisha tunawapa burudani mashabiki wa klabu hiyo kwa kuwapa kile ambacho kinafanywa na klabu yao hiyo," alisema Mhando.

Bosi huyo alisema wataendelea kuongeza ubora ndani ya miundombinu ndani ya klabu hiyo kwa ajili ya kuhakikisha soka la Tanzania linaendelea kupata mafanikio.

"Pia kutakuwa na gawio la asilimia kila mwisho wa mwezi kwa msimu, watakuwa wanapokea Sh. milioni 200 kwa mwezi na kwa kila msimu kiasi cha fedha kitakuwa kinapanda hadi msimu wa mwisho wa mkataba wao watapokea Sh. milioni 380," alisema Mhando.

Aliongeza mbali na kuonyesha matukio yao kwenye televisheni, kila mwaka kuanzia msimu wa 2021/22 klabu hiyo itakuwa inapokea kiasi cha Sh. bilioni tatu kutoka Azam TV kama watamaliza Ligi Kuu wakiwa katika nafasi mbili za juu 'Top 2'.

Naye Msolla alisema klabu yake inaahidi kutimiza makubaliano yaliyofikiwa ili shughuli za klabu hiyo zifanyike kwa ufanisi na kuhakikisha maendeleo ndani ya klabu hiyo yanapatikana.

"Hili jambo halikuwa rahisi, tutakaa uongozi na kwenda kutoa semina kwa mashabiki wetu kupitia matawi kuwapa elimu na kuwaeleza kuhusu mkataba huu," alisema Msolla.

Alisema mkataba huo unaonyesha jinsi Yanga ilivyokuwa kubwa hapa Tanzania na kuainisha haki kwa kila upande kwenye makubaliano hayo yaliyofikiwa.

Kwa sasa Yanga iko katika nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa na pointi 70 na imebakiza michezo miwili ili kumaliza msimu.

Watani zao na mabingwa watetezi, Simba ambao msimu huu walifika hatua ya robo fainali ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika wanaongoza katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara wakiwa na pointi 76 na wanahitaji pointi moja kwenye michezo yake mitatu iliyobakia ili kutwaa taji hilo kwa mara ya nne mfululizo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002